# *Yesu Kristo Yeye Yule Jana, Leo, Na Hata Milele*

Mbarikiwe. Asante, bwana. Vizuri sana kuwa hapa usiku wa leo. Nimeungojea wakati huu kwa matarajio makubwa. Tulikuja kwenye mji wenu mzuri yapata miezi sita iliyopita, mara baada ya Krismasi, na tumekuwa tukikaa hapa pamoja nanyi. Basi siku moja wakati tukiwa nje na Ndugu Tony Stromei, Mimi . . . Tuliingia wazo ya kwamba ingekuwa ni vizuri kufahamiana vizuri zaidi kabla haijatubidi kuondoka. Ndipo tukafikiria ingekuwa vizuri kuwa na uamsho mdogo hapa chini, kupata ninii . . . sote tukusanyike pamoja na kuwa na ushirika kwenye Neno la Mungu. Na mimi . . .

2 Wengi wa hawa ndugu nimekutana nao, nami nikayatembelea baadhi ya makanisa yao na kupata makaribisho mazuri mno. Na ninafikiri ni jambo zuri sana kwamba tunaweza kukutana sote pamoja kwa siku hizi chache usiku sasa, kuwa na ushirika katika Neno la Mungu. Tunatumaini ya kwamba itakuwa ni fanaka kubwa kwa ajili ya utukufu wa Mungu, na kuijenga huduma ambayo Yesu aliifia, hiyo ni, kwamba aweze kuwa na kanisa bila waa wala kunyanzi hapo Yeye atakaporudi. Sasa, hatuwakilishi dhehebu lolote lile. Tunakuja tu kama wa baina ya madhehebu, kukusanyika pamoja na kila Mkristo, ili tuweze kuwa na ushirika huu pamoja.

3 Pia tunaenda kuwaombea wagonjwa. Na mara nyingi, unapotaja kuwaombea wagonjwa, basi wanasema, "mponyaji wa Kiungu." Hapana. Siamini yupo ila Mmoja, na huyo ni Kristo. Sisi . . . Wakati mwingine wanakubandika hilo, kama mponyaji wa Kiungu, bali kwa sababu unawaombea wagonjwa. Bali siamini kwamba kuwaombea wagonjwa kungekufanya zaidi sana mponyaji wa Kiungu kuliko ingekufanya wewe Mwokozi wa Kiungu kuwaombea waliopotea. Kwa hiyo tunajua kwamba tusingekuwa Mwokozi wa Kiungu wala mponyaji wa Kiungu.

4 Tunaamini ya kwamba fadhila hizi zote tunazofurahia siku hizi katika uchumi huu wa Ukristo tulio nao, zote zilinunuliwa pale Kalvari na Mwana wa Mungu, Yesu Kristo. Tunaamini ya kwamba "Alijeruhiwa kwa makosa yetu. Alichubuliwa kwa maovu yetu. Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa mapigo Yake sisi tuliponywa." Yote ni wakati uliopita. Ni jambo ambalo Mungu ametufanyia pale Kalvari. Ndipo, kama Wakristo, tunayo haki ya kufurahia baraka hizi ambazo Yeye ametununulia.

5 Kwa hiyo, basi, hakuna mtu angaliweza kumwokoa

mwingine. Kama ingalikuwa hivyo, Yesu isingalimbidi kufa. Bali wakati Yesu alipokufa pale Kalvari, Yeye alilitatua swali la dhambi milele. Basi kila mtu, kila kiumbe duniani, wakati Yeye alipokufa, kiliokolewa dakika iyo hiyo. Kila . . . Gharama ililipwa, kikamilifu. Ilitimizwa sana hata Mungu akatambulisha ya kwamba ilikuwa kweli.

6 Sasa, jambo pekee litupasalo kufanya, kuipokea hii, ni kuikubali, kuiamini na kuikubali. Bali haijalishi Yeye alikufa kiasi gani kwa ajili ya wokovu wetu, ha—hatuna budi, sisi wenyewe, kulikubali kama tukio letu wenyewe binafsi, sha—shauku yetu wenyewe. Ni lazima tuwe tunataka kuokolewa, na kuamini ya kwamba juu ya msingi wa Damu Yake iliyomwagika ya kwamba tumeokoka tukiisha kutimiza masharti ya Biblia.

7 Ninaamini katika Biblia kuwa ndiyo ufunuo mkamilifu wa Yesu Kristo. Sasa, ninaamini ya kwamba Mungu anaweza kufanya mambo ambayo hayajaandikwa katika Biblia, kwa sababu Yeye ni Mungu. Lakini mradi tu tunaweza kulipata katika Biblia, kama ahadi, basi tunajua ni kweli, kwa sababu Ne—Neno ni kweli, daima. Na kwa hiyo tunamwamini Yeye kutimiza ahadi Yake.

8 Ninaamini ya kwamba Yeye ni mwenyezi. Ninaamini Yeye hana kikomo. Akiwa hana kikomo, Yeye alijua mambo yote. Yeye anajua mambo yote. Miaka milioni moja kabla hakujakuwako na ulimwengu, Yeye alijua tungeketi papa hapa usiku wa leo. Kama sivyo, Yeye si asiye na kikomo. Na kama Yeye—na kama Yeye si asiye na kikomo, basi Yeye si Mungu.

9 Kwa hiyo tunaamini kwamba Neno, Biblia hii, ni Neno la Mungu, na, kwa hivyo, kwamba—kwamba unaweza kuining'iniza nafsi yako juu ya fungu Lake lolote. Hiyo ndiyo njia pekee uwezayo kuwa na imani, ni kuamini una ninii . . . Imani haina budi kuwa na mahali pa kutia nanga mahali fulani, nayo haina budi kutia nanga mahali fulani. Na hakuna kitu kingaliweza kuwa imara zaidi ya Neno la Mungu, kwa sababu Neno ni Mungu. Hivyo ndivyo Biblia inavyofundisha. Kwa hiyo, Mungu anaposema jambo lolote Hapa ndani, mwaminio anaweza kuliitikia Hilo kwa "amina," lolote Yeye asemalo.

10 Sasa, kwa sababu Yeye kuwa ni asiye na kikomo, mwenye nguvu zote, aliye mahali pote, Yeye hawezi kuwa moja bila hiyo nyingine. Na ili apate kuwa ni Mungu, hana budi kuwa hizo zote.

11 Sasa, hivyo basi, tukiwa wenye kikomo jinsi tulivyo, mwaka huu tunaweza kushughulikia jambo fulani na tunafikiria tumelifanya kikamilifu. Mwaka ujao, ama labda kesho, hatuna budi kubadilisha nia zetu. Ni tofauti. Tumepata jambo bora zaidi, kwa sababu, sisi, tuna kikomo.

12 Lakini Yeye hana kikomo. Kwa hiyo Yeye anaposema Neno, ni hivyo daima. Kamwe haliwezi kuboreshwa. Haliwezi kughairiwa. Kama Mungu aliitwa jukwaani, katika kisa

chochote, basi jinsi Mungu alivyofanya kwenye tukio hilo, mara ya kwanza, Yeye hana budi kufanya vivyo hivyo daima hapo anapoitwa jukwaani tena.

13 Kwa sababu, kama angefanya tofauti na vile alivyofanya mara ya kwanza, basi kuna kasoro fulani. Mnaona? Yeye. . . Isingeweza kuwa kamilifu. Mnaona? Kwa hiyo Yeye alifanya vibaya wakati alipofanya mara ya kwanza, kama akifanya mara ya pili tofauti na vile alivyofanya mara ya kwanza.

14 Hivyo basi, wakati Mungu alipofanya suluhisho kwa mtu kuokolewa, katika bustani ya Edeni. Yeye. . .Walijaribu kuboresha suluhisho Lake, kupitia miaka elfu sita, wala hawawezi kuligusa. Yeye alifanya, juu ya msingi wa Damu ya mhanga asiye na hatia, na Yeye kamwe hajaibadilisha. Tumejaribu kuwaelimisha watu kwa Kristo. Tumejaribu kuwafanyizia dhehebu kwa Kristo. Tumejaribu kila namna ya mifumo, lakini yote imeshindwa. Kuna mahali pamoja tu ambapo mwanadamu anaweza kukutana katika mahali shirika, na kuabudu, na hapo ni chini ya Damu iliyomwagika ya Yesu Kristo. Imekuwa hivyo tangu mwanzo, maana Yeye hawezi kupabadilisha. Daima ni Damu, Damu.

15 Basi leo hii tunapowazia ya kwamba sisi ni tofauti na jamaa huyo mwingine, na kadhalika, kamwe haifanyi kazi. Hatuna budi kuendelea kukubali msingi huo wa Damu iliyomwagika. Na kwa hiyo, hapo Mungu alipoitwa jukwaani, kumponya mwanadamu, Yeye alimponya mwanadamu juu ya msingi wa imani yake. Basi wakati Yeye anapoitwa jukwaani tena, Yeye atamponya mtu huyo mwingine jinsi iyo hiyo, la sivyo alitenda vibaya. Kama Mungu alipata kumponya mtu kwa sababu aliamini, na kisha mtu huyo mwingine anamwita kwa imani ile ile, Mungu anawajibika kufanya jambo lile lile kwa mtu huyo mwingine. Kama sivyo, Yeye ana upendeleo, na alifanya vibaya hapo kwanza. Kwa hiyo, mnaona, turudi kwenye Neno. Ni—ninaliamini kwa moyo wangu wote.

16 Sasa tunamtarajia Mungu kufanya mambo makuu kwa ajili yetu. Nasi tunataka, tutakapoondoka, kuona baraka imeachwa katika jiji hili. Nami najua mtakuwa baraka kwangu, kwa kuwa popote wawili au watatu wamekusanyika katika Jina Lake, Yeye aliahidi kuwapo. Sasa, kama hivyo sivyo, basi sote tumepotea na Biblia imekosea. Hilo linamfanya Yesu Kristo hapa sasa. Kama hivyo sivyo ilivyo, basi tunahubri nini, tunaamini nini? Mnaona? Yeye yupo hapa. "Walipo wawili au watatu wamekusanyika katika Jina Langu, Mimi niko miongoni mwao." Sasa, hatuna budi kutenda basi, na kuamini, na—na kuamini ya kwamba Yeye yupo hapa, na kutenda kana kwamba Yeye yupo hapa. Pia kumbukeni, Yeye hutulinda baada ya sisi kuondoka hapa, pia.

17 Nasi tunatumaini ya kwamba kila mtu asiyeokoka ataokoka kwenye uamsho huu. Tunatumaini ya kwamba hapatakuwapo na kiti kitupu, katika kila moja ya makanisa haya hapa ambayo

yamewakilishwa, tangu sasa na kuendelea. Nami ninatumaini ya kwamba patakuwapo na uamsho wa mtindo wa kale uliotumwa na Mungu, utakaotokea, kupitia hapa Tucson, ambao utapeleka maelfu ya watu katika Ufalme wa Mungu. Ninaamini hayo ndiyo mapenzi ya Mungu. Hiyo ndiyo shauku Yake usiku wa leo.

18 Na hakuna mtu mmoja anayeweza kufanya jambo hilo kwa nafsi zao wenyewe. Inahitaji sisi sote, pamoja, kushirikiana, kuomba pamoja, kusimama pamoja katika umoja, katika Roho. Na kuombea hili. Ndugu wamekuwa wakiniambia ya kwamba makanisa yamekuwa na mikutano ya maombi, kabla ya mkutano huu. Nami ninashukuru sana kwa jambo hilo. Litaninii... Mnapokusanyika pamoja kuomba namna hiyo, inabadilisha hali yote ya mambo, tunapoomba.

19 Sasa, hatutajaribu kuwaweka kwa muda mrefu, katika kila jioni, kwa sababu ninajua hamna budi kutoka na kwenda kazini mwenu. Hivyo basi tutajaribu, kila usiku, kuwaachilia mapema, ili mweze kurudi kesho yake usiku. Na hii ni ziara fupi tu, vile tumekusanyika. Nasi tuna siku nne tu usiku, ninaamini. Ni, nafikiri, hiyo ni kweli, Jumatano, Alhamisi, Ijumaa. Naam. Vema, siku nne usiku. Na ndipo tunamalizia hapa katika jumba lili hili la mikutano kwa ajili ya kiamshakinywa cha Wafanyabiashara, Jumamosi asubuhi, ambapo, watu wote wamekaribishwa.

20 Sasa, mimi si mgeni. Sijisikii kama mgeni miongoni mwenu. Mimi ni—mimi ni ndugu yenu. Na kwa hiyo natumaini ya kwamba mnajisikia vivyo hivyo kunihusu mimi. Na sasa, kabla hatujalikaribia Neno, hebu na tumkaribie Mwandishi wa Neno huku tukiinamisha vichwa vyetu kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi.

21 Mwenyezi Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Yule aliyemfufua kutoka kwa wafu na amemdumisha hai miaka hii yote...Na Yeye yu hai milele akitawala mioyoni mwetu usiku wa leo, akichukua mamlaka, kutuongoza na kutuelekeza. Jalia sisi sote tujisalimishe kwa mapenzi Yake ya Kiungu, ili Yeye aweze kutuongoza katika njia ambayo angetaka tuiendee.

22 Tunataka kukushukuru Wewe, Baba, kwa ajili ya nafasi hii ya ajabu kumwasilisha Yesu Kristo katika njia ya Mponyaji mkuu mwenye nguvu, Mwokozi mkuu wa mwanadamu, Mtoshelezaji wa kila moyo wenye shauku, Afya kwa wagonjwa, Wokovu kwa waliopotea, Mfalme ajaye kwa watakatifu. Ee Mungu, tuvuvie sote, usiku wa leo.

23 Ninakushukuru Wewe kwa ajili ya watu hawa, wachungaji hawa wa makundi ya jiji hili, hawa ndugu wahudumu ambao wana vituo vyao vidogovidogo kote jijini, ambako wanatamani sikuzote kwamba Roho wa Mungu aje katika ma—mawimbi ya—ya Roho Mtakatifu, aingie miongoni mwao na kuwaambia liwapasalo kufanya, jinsi iwapasavyo kuwaongoza kondoo. Basi

usiku wa leo, inaonekana, Bwana, wakati Ujumbe ulipoingia upesi kupitia kwa mawimbi hayo, kwamba wote walikubali kwamba hatuna budi kuja pamoja katika ibada hii. Sasa njoo, Bwana Yesu.

24 Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya Hoteli hii ya Ramada na kwa ajili ya mikono yake iliyo wazi kuipokea Injili, kuturuhusu kuja hapa kuabudu katika jengo hili lenye hali nzuri ya ubaridi. Baba Mungu, tunaomba ya kwamba hakutakuwako na mtu aliyepotea atakayetoka kwenye jengo hili pasipo kuokolewa. Tujalie, Bwana. Jalia ninii . . . Kama watumishi wa jengo hili, katika Ramada hii kuu, hawajaokoka, tunaomba, Mungu, kwamba utawaokoa.

25 Ponya magonjwa pote hapa. Jalia itimie kwamba watu watatembea kwenye jumba hili la mikutano na kulia, chini ya nguvu za Roho Mtakatifu. Tujalie, Bwana. Tuna shauku kwa ajili ya mambo haya. Nasi tunaamini ni mapenzi Yako ya Kiungu kutufunulia hayo sasa, na kutuonyesha Uwepo Wako, kwamba Wewe upo hapa na uko hai daima, na pamoja nasi milele.

26 Tubariki tunapotia bidii yetu dhaifu. Jalia Roho Mtakatifu aingie. Pia jalia tusiwaze mawazo yetu wenyewe, bali jalia nia zetu ziwe wazi kuukaribisha upako mkuu wa Uwepo Wake, kusudi tujue nia Yake, kuyatimiza yaliyoandikwa katika Maandiko, "Nia iliyokuwamo ndani ya Kristo na iwe ndani yenu."

27 Tubariki, Baba yetu. Na wakati tutakapoondoka kwenye ibada usiku wa leo, jalia tuseme tunapoenda nyumbani kwetu, "Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo aliposema nasi njiani?" kama ilivyofanya siku moja zamani za kale, kwa shahidi wa kwanza wa ufufuo, wakati Kleopa na rafiki yake walipokuwa wakirudi kutoka mjini. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

28 Watu wengi kwa namna fulani huchukua Maandiko ambayo mwinjilisti ange—angeyasoma. Nami ningependa, usiku wa leo, kuchukua tu vifungu vichache vya Maandiko na kujaribu kuvielezea, kwa njia yangu nyenyekevu, kusudi mweze kumwona Yesu Kristo. Nawatakeni mfungue pamoja nami sasa kwenye kitabu cha Yohana Mtakatifu, mlango wa 12 na kifungu cha 20, kama mngetaka kunifuata tunaposoma. Yohana Mtakatifu 20 ama . . . Yohana Mtakatifu 12:20 na 21.

> *Palikuwa na Wayunani kadha wa kadha miongoni mwa watu waliokwea kwenda kuabudu kwenye sikukuu:*
>
> *Basi hao walimwendea Filipo, mtu wa Bethsaida ya Galilaya, wakamwomba, wakisema,* Mabwana, *sisi tunataka kumwona Yesu.*

29 Halafu katika kitabu cha Waebrania, mlango wa 13 na kifungu cha 8.

*Yesu Kristo yeye yule jana, . . . leo, na hata milele.*

30 Ninataka kulifanya hili kama somo: *Yesu Kristo Yeye Yule Jana, Leo, Na Hata Milele.*

31 Nilikuwa nikihudhuria kanisa Jumapili usiku, hapa jijini, moja ya makanisa yenu mazuri. Na hapa nimejaribu kuyatembelea mengi niwezavyo, tangu tumekuwa hapa jijini, na kupata ushirika mkubwa na makaribisho kwenye Assemblies of God, Wabaptisti, na Anderson Church of God, na mengi zaidi niliyotembelea. Na kwenye kanisa hili, nyuma ya—ya mimbara, palikuwa na Maandiko, kama Biblia, yameandikwa, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Hilo kwa namna fulani limekuwa ndilo wazo langu katika miamsho, kwamba ningetumia hilo, kwa sababu ninaamini Kitabu kizima ni ufunuo wa Yesu Kristo, na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Na halafu kwa . . .

32 Ningetaka kujenga kwa ajili ya somo langu, "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Na mimi—mimi ninaamini, usiku wa leo, ya kwamba kila mwanamume na mwanamke hapa ndani angejisikia kwa njia huru kwamba hawa Wayunani walielezea hisia zetu sote. Kwa kuwa, walikuwa wamesikia habari za Yesu, na sasa walitaka kumwona. Ni—ninaamini kwamba—kwamba hakuna mtu anayeweza kusikia hadithi ya ajabu ya Yesu Kristo ila kwamba atakuwa na hamu moyoni mwake kuweza kumwona. Hiyo ni—ni . . . Hiyo ndiyo—ndiyo shauku ya mwaminio, ni kumwona Yeye. Na mimi sijali kama Yeye ni mfupi, mrefu, ama Yeye ni nini. Ninampenda. Ninataka kumwona. Na Yeye Yule aliyeniokoa na amenifanyia yale amefanya, ni—ninatamani kumwona.

33 Sasa, hapana shaka ya kwamba Wayunani hawa walikuwa waongofu wa dini ya Kiyahudi, kwa sababu tunaona ilikuwa ni sikukuu ya Pasaka, ambapo mwana-kondoo wa pasaka alichinjwa, na hawa Wayunani wakiwa ndani miongoni mwao. Sasa, Wayunani walikuwa watu wenye vipaji sana. Walikuwa wanauongoza ulimwengu kwa sanaa. Nao wameelimika sana katika sayansi. Pia walikuwa ni watu mashuhuri. Na walikuwa ni wasomi; walisoma vitabu vingi. Na—na jambo fulani, hapana shaka walikuwa wameshika ki—kitu fulani; kwamba katika moyo wa mwanadamu, wakitamani kupata kitu fulani kinachoridhisha hicho kiu kikuu kinachoingia moyoni mwa mwanadamu.

34 Uliwahi kuwazia ni kwa nini mwanadamu angefanya kosa? Ni kwa sababu anajaribu kuridhisha kiu ambacho Mungu aliweka moyoni mwake, kumwonea Yeye kiu. Ndipo basi anajaribu kukiridhisha kwa mambo ya ulimwengu. Kamwe hakitaridhishwa mpaka kizimishwe na Mungu Mwenyewe, mpaka anapoweza kuingia na kuridhisha shauku hiyo kuu pamoja na kiu katika moyo wa mwanadamu. Kuna kiasi kikubwa sana cha mwanadamu ambacho hakitatosheka.

Hakuna kitu kingine kinachoweza kuchukua mahali pake mpaka Mungu achukue mahali Pake halisi katika moyo wa mwanadamu.

35 Nao hawa Wayunani walikuwa wamesikia, na hapana shaka walikuwa wakisoma Agano la Kale, nao walikuwa wamesikia kuhusu Masihi ajaye na kile angekuwa atakapowasili. Nao walikuwa wametamani kuona kile Mungu angekuwa wakati angedhihirishwa katika mwili, jinsi Mtu angeonekana ambaye angejazwa hadi pomoni mpaka utimilifu wa Uungu ungekuwa ndani Yake. "Angekuwa nini?" Nao walikuwa wamesikia habari za Yesu, ambaye alidai kuwa Mtu huyu, yule Masihi.

36 Ambaye, Wayahudi kwa maelfu ya miaka walikuwa wamemtarajia Huyu ajaye, ambapo Mungu Mwenyewe angefanyika mwanadamu katika mfano wa Mwana Wake, kusudi apate kutokwa na damu na kufa. Kwa kuwa hapakuwapo na mtu angaliweza kufa kwa ajili ya mwingine, kwa sababu sote tulikuwa na hatia, pamoja. Mtu mmoja asingeweza kumwokoa mwingine.

37 Na ilibidi kuwepo na Mtu aliyestahili. Katika torati za kale, ambazo wahudumu wanajua, kama mkombozi wa jamaa. Ilikuwa . . . Yeye, Mungu, ilibidi awe wa Jamaa yetu. Naye akavuka he—hema Lake. Ndipo akashuka chini, kutoka kuwa Mungu, yule Yehova mkuu; akafanyika mwili, katika umbo la Mwana Wake, ili Mungu aweze kudhihirishwa. Na awe mstahilifu, na Jamaa yetu, kusudi Yeye aweze kufa ili kuziondoa dhambi zetu, kuokoa viumbe Wake Mwenyewe.

38 Loo, hadithi hiyo ni kuu sana! Hakuna njia ya kuiendea, kujua halisi, jinsi ungeweza kuielezea. Hakuna . . . Halipo katika ulimi wa mwanadamu, ambalo lingeweza kuelezea huo ni upendo wa jinsi gani, kwamba Mungu angeweza kushuka chini, Mwumba, apate kuwaokoa viumbe Wake Mwenyewe.

39 Sasa, tunaona hawa Wayunani wakiona kiu. Walikuwa wamesikia. "Imani chanzo chake ni kusikia, na kulisikia Neno." Biblia ilisema hivyo. Waebrania ilisema, "Imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia Neno la Mungu." Sasa, walikuwa wamesikia ya kwamba kulikuwa kuwe na Masihi, kwa hiyo basi wakaja kuona. Wao, walikuja kumwona Mtu huyu aliyekuwa awe huyo Masihi; Yule aliyeaminiwa, miongoni mwa watu, alikuwa yule Masihi.

40 Sasa, hapo ni mahali pale pale ambapo tumeketi usiku wa leo. Tumesikia kuhusu Mungu. Tumefundishwa kuhusu Mungu. Kote katika miaka, tumekuwa na makanisa, makanisa makuu, watu mashuhuri, wainjilisti mashuhuri. Bali ninaamini tunaishi katika kivuli cha Kuja kwa Bwana Yesu. Wakati, Kanisa hili limekuja kutoka kuhesabiwa haki chini ya Luther, kutakaswa chini ya Wesley, likaingia katika ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kufikia Kanisa kamilifu bila waa wala kunyanzi. Ili, kupitia

Kanisa hilo, Mungu aweze kuwakomboa tena watakatifu wote waliooshwa kwa Damu, na kuwapeleka Nyumbani, kote katika nyakati. Na sisi ndio . . . Tunafanyika zaidi kama Kristo, na kuwa katika uchache zaidi, wakati wote.

41 Sasa, tunaona ya kwamba watu hawa wakiwa na njaa, walikuja kuona alivyoonekana Mtu huyu. Nao wakauliza swali, "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Sasa, walikuwa wamesikia habari Zake, wakawasikia wengine wakinena juu Yake, wakasoma habari Zake katika Biblia, bali walitaka kumwona.

42 Sasa kwenye fungu langu, Biblia ilisema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Halafu, kama watu hawa walitaka kumwona, naye Mungu akafanya njia ili kwamba matarajio yao yaridhishwe; alifanya njia ili waweze kumwona Yeye, kwa mmoja wa watumishi Wake. Sasa, ikiwa—ikiwa Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, nasi tuna shauku ile ile aminifu ya kumwona, hivi si anawajibika kujionyesha Mwenyewe miongoni mwetu? Sasa, hilo ni tamshi kubwa zito. Lakini kama Biblia si kweli, basi tuko wapi? Mnaona? Lakini Biblia ilisema Yeye ni yule yule. Na kama Yeye . . . Hawezi kuwa tu yeye yule katika njia *fulani*. Hana budi kuwa ni yeye yule kwa kila njia ambayo aliwahi kuwa. Yeye anasema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele."

43 Nao hawa Wayunani walitaka kumwona, kwa sababu imani ilikuwa imekuja kwa kusikia. Nao wakaja na wakatoshelezwa. Wakaondoka, wakijua ya kwamba huyo alikuwa ndiye Masihi.

Sasa, kama tunatamani usiku wa leo kumwona Huyu Ambaye . . .

44 Tunaenda kanisani, kama tunajisikia kwenda ama hatujisikii; na ambapo sisi, kanisa letu, tunatoa zaka zetu. Je! ni—ni kwa hadithi ya kubuni? Je! ni je—jengo tu ambalo tunalipia? Hivi mtu huyu, ambaye ni mchungaji wetu, ni mwigaji tu wa kitu kisicho na maana yoyote? Hivi dini ya Kikristo ni kama hadithi ya kubuni ya Kiyunani ama hadithi ya kubuni ya Kirumi, ama kitu fulani, ni hadithi tu ya kubuni? Ama, ni uhalisia?

45 Sasa, kwangu mimi, Biblia hii ama ni kweli au ni ya uongo. Kila Neno ni kweli ama hakuna lolote la Hiyo lililo kweli. Mnaona? Na sasa, kama Yeye alifanya ahadi hii, basi si mimi na wewe tunaowajibika kwa ahadi hii. Si mimi na wewe tunaowajibika kuthibitisha ahadi hii. Yeye Ndiye anayewajibika, kwa sababu Yeye alikuwa Ndiye aliyelisema. Kweli. Sisi tunanukuu tu yale Yeye aliyosema, ya kwamba, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Na hii hapa . . .

46 Ni wangapi hapa wangetaka kumwona? Kwa ku—kusema tu, inua mkono wako. Sema, "Na—napenda . . . " Sasa, kulikuwako na wawili pale, wawili tu waliotaka kumwona, na hawa hapa

mia mbili ama mia tatu wanaotaka kumwona. Vema, basi, kwa nini hatuwezi kumwona kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele? Sasa, hivyo ndivyo tunavyotaka kuliangalia. Ama ni Kweli au si Kweli. Na hiyo ndiyo sababu nililieleza mara ya kwanza. Biblia hii ama ni Kweli au si Kweli. Hivyo basi, Biblia inaposema lolote, unaweza tu kulishikilia, kwa kuwa Mungu anawajibika kwa Neno hili, kwa kuwa Yeye Ndiye aliyeifanya ahadi. Mungu alisema hivyo, vema, ni kweli.

47 Sasa, itategemea kile unachotafuta. Kwa kawaida unapata kile unachotafuta. Ninawatakeni mkumbuke hilo. Sasa, kama mkitaka kumwona Mungu, Mungu anaweza kuonekana. Kama unataka kumsikia Mungu, Mungu anaweza kusikiwa. Kama tu alivyokuwa jana, ndivyo alivyo leo. Habadiliki.

Sasa, inanikumbusha hadithi ndogo, hata hivyo ni ya kweli.

48 Ninaishi Indiana, nchi ya uenyeji wangu. Mimi ni Mkentaki, kwa kuzaliwa. Nasi tunaishi karibu na Mto Ohio. Maji ya kutosha hupitia kule, siku moja, kuzifanya saladi zikue kote Arizona. Mamilioni ya galoni za maji huteremka kupitia kwenye bwawa hilo, na inaonekana kana kwamba kwa njia fulani tungeyakwepa. Tuna zaidi ya tunayohitaji kule. Karibu ni kinamasi. Na—nanyi mnayahitaji hayo maji hapa. Lakini itakuwa, siku moja, katika ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu ujao, wakati dhambi itakapoondolewa duniani, nayo mambo yatakuwa sawa.

49 Kulikuwako na mzee mvuvi aliyeishi kule chini kwenye mto huo. Alikuwa ni shemasi kanisani mwangu. Jina lake lilikuwa Wiseheart, mzee mzuri sana. Basi kulikuwa na shule fulani ya Jumapili mjini mwetu, kanisa zuri, dhehebu zuri kubwa linalojulikana kote ulimwenguni, ushirika, mchungaji mzuri, na watu wazuri. Na kulikuwako na familia fulani mjini mwetu, ambayo ilihudhuria kanisa hili. Na kulikuwako na mvulana mdogo katika familia hii aliyechochewa sana siku moja, baada ya kusikia masomo mengi yaliyoandikwa yakisomwa na kadhalika, mpaka akamwambia mama yake, akasema, "Mama, ikiwa Mungu ni Mungu mkuu, kama usemavyo ndivyo alivyo, mtu yeyote anaweza kumwona?"

50 Akasema, "Mwanangu, unapaswa kumwuliza mwalimu wako wa shule ya Jumapili. Mama hawezi kukwambia hilo."

51 Kwa hiyo akamwendea mwalimu wa shule ya Jumapili na akasema, "Mwalimu, ningetaka kukuuliza jambo fulani. Wewe huniambia juu ya Mungu mkuu," kasema, "ambaye ni mkuu sana. Yeye huifungua Bahari ya Shamu kwa Israeli. Pia hulifanya jua kuwaka, na kuizungusha dunia kasi kwa wakati mkamilifu, kwenye mzingo wake, na kadhalika." Kasema, "Je, mtu yeyote anaweza kumwona?"

52 Akasema, "Hilo ni la kilindi sana kwangu. Itakubidi kumwuliza mchungaji."

53 Kwa hiyo akafika kwa mchungaji na akasema, "Mchungaji, je! mtu yeyote anaweza kumwona Mungu?" Kasema, "Yeye ni mkuu sana. Nasikia wewe huzungumza kutoka Kwake, kutoka mimbarani, ukisema jinsi Yeye alivyo mkuu." Kasema, "Hivi mtu yeyote anaweza kumwona?"

54 Kasema, "La, mwanangu. Hakuna anayeweza kumwona Yeye," kasema, "kwa sababu huwezi kumwona Mungu. Hivyo tu. Inatubidi tu kuamini."

55 Vema, maskini jamaa huyo, halikumridhisha. Kwa hiyo yeye, siku moja, alikuwa pamoja na huyo ndugu mzee, mvuvi, mtoni. Nao walikuwa wameenda kwenye kile kinachoitwa Kisiwa cha Maili Sita. Ni maili sita, kisiwa, kutoka Louisville, Kentucky, mpaka kisiwa hiki. Walikuwa wakivua samaki kule juu, nao walikuwa wamewavua samaki wengi. Basi wakiwa njiani kwenda zao, ikatokea tufani. Na huko tuna tufani nyingi, nchi—nchi hiyo yenye mvua nyingi, radi na ngurumo, na mabubujiko makubwa ya mvua. Na—na kwa hiyo baada ya . . . Iliwabidi kwenda ufukoni na kwenda nyuma ya miti.

56 Ndipo baada ya tufani hiyo kwisha, wakarudi kwenye mtumbwi wao na kuanza kuteremka. Ilikuwa ni wakati wa jioni, ama alasiri, hasa, nalo jua likitua huku nyuma Tucson mahali fulani. Lilikuwa likiakisi nuru yake angani, na kulikuwako na upinde wa mvua uliotokea kwenye upeo wa macho wa mashariki. Basi maskini yule mvuvi alikuwa akipiga makasia mtumbwi wake kwa makasia yake. Kwa kuwa, kila kitu ni shwari, mvua ilikuwa imefagilia mbali mavumbi, na ni wakati mzuri sana. Na ni mtu tu ambaye amezoea makasia anayeweza kuthamini uwiano huo wa kuinamisha makasia, huku mtumbwi ukitambaa ukienda zake majini. Huku ndevu zake zenye mvi zimening'inia chini, naye akaendelea kuangalia upinde huo wa mvua.

57 Ndipo maskini mvulana huyo, mwenye shauku, akaangalia kila mahali aone ni nini huyo mzee muungwana alikuwa akiangalia. Basi akamwona maskini mvuvi huyo, machozi ya fuele yakitiririka kwenye ndevu zake zenye mvi. Ndipo maskini mvulana huyo, akiketi kwenye gubeti la mtumbwi, alishikwa sana na shauku hata akakurupuka kwenda kwenye shetri ya mtumbwi na kumwambia mzee mvuvi, "Bwana, nitakuuliza swali ambalo mama yangu, wala mwalimu wangu wa shule ya Jumapili, wala mchungaji wangu angeweza—angeweza kuridhisha shauku yangu ya kujua jambo fulani."

Akasema, "Ni nini, mwanangu?"

Akasema, "Je! mtu yeyote anaweza kumwona Mungu?"

58 Ndipo huyo mzee mvuvi, amelemewa sana na ninii yake . . . swali la jamaa huyo mdogo, aliyavuta makasia ndani ya mtumbwi, akamkumbatia mvulana huyo mdogo. Nayo machozi yakatiririka mashavuni mwake. Akasema, "Mungu aubariki

maskini moyo wako, kipenzi. Yote ambayo nimeona, kwa miaka hamsini iliyopita, imekuwa ni Mungu." Naam. Mnaona?

59 Unaweza ukampata Mungu kwa wingi sana, upande wa ndani, hata unaweza kumwona kila mahali uangaliapo. Mnaona? Lakini mpaka uifikie hiyo shauku ya kumwona, hutamwona. Unaweza kumwona katika kutua kwa jua. Unaweza kumsikia katika mlio wa ndege. Unaweza kumwona kila mahali. Yuko kila mahali. Lakini mzee huyo alikuwa na Mungu kwa wingi sana, ndani yake, a—angeweza kumwona Mungu kila mahali. Nami nafikiri kwa namna fulani hivyo ndivyo tunavyopaswa kumtafuta Mungu, ndipo tunaweza kumwona Mungu kila mahali tunapoangalia.

60 Sasa, lakini, tumerudi kwenye, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Sasa, tunge—tungejuaje?

Kama nilisema, "Enyi Wamethodisti, mnaamini hilo?"

Wangesema, "Amina."

Nami ningesema, "Baptisti, mnaamini hilo?"

"Amina."

61 "Wapentekoste, church of God, na kadhalika, mnaamini hilo?"

62 "Amina. Tunaliamini." Nami nina furaha mnaliamini. Ninaliamini, pia.

63 Lakini, sasa, vipi kama tungaliuzunguka mji, kumtafuta Yesu Kristo, tungemtafuta Mtu wa aina gani? Sasa, Yeye aliahidi kuwa pamoja nasi usiku wa leo. Sasa, kama sivyo ilivyo, basi Neno si la kweli.

64 Mnasema, "Vema, Hilo kamwe halijatiwa pumzi." Basi, kwangu mimi, hayo mengine hayajatiwa pumzi. Sijui ni lipi lililo ama lile lisilo na pumzi, kama lote si Kweli. Mnaona? Siwezi kulichagua.

65 Lote tu ni Neno la Mungu. Basi sasa—sasa, Yeye aliahidi ya kwamba angekuwa papa hapa usiku wa leo, "Popote walipo wawili au watatu wamekusanyika pamoja." Mnaamini hilo? Asanteni.

66 Sasa, basi, kama ndivyo alivyo, tungemtafuta Mtu wa aina gani, kama tulienda kumtafuta Yeye? Hivi tunge—hivi tungejaribu kumtafuta mtu aliyevaa joho na alikuwa na nywele ndefu na ndevu? Huyo angekuwa, huyo angeweza kuwa, ni Yesu? Mtu yeyote tu angeweza kuvaa jo—joho na kuwa na nywele ndefu na ndevu. Mwigaji yeyote angeweza kufanya hivyo. Wapo watu wengi wanaovaa joho usiku wa leo, wasiojua zaidi kuhusu Mungu kuliko Mhotentoti angejua kuhusu hekaya za Kimisri. Hiyo ni kweli. Lakini hilo—hilo silo tungetarajia.

Tunatarajia, tunataka mwungwana fulani, kwa sababu Yeye hakuwa.

67 Tungetafuta nini, makovu ya misumari na alama za miiba? Mwigaji yeyote anaweza kujivalisha namna hiyo. Ingali isingekuwa ni Yeye.

68 Basi tunajuaje kwamba alikuwa amevaa jo—joho, na jinsi alivyovalia? Tunajua tu . . .

69 Angefanana na picha tunazoona, wa—wachoraji wanazochora? La. Huo ni mchoro wa kisaikolojia ambao mtu fulani alikuwa nao, dhana yake ya jinsi Yesu angeonekana. Na kama ingalitubidi kuitegemea hiyo, ni yupi angekuwa sahihi? Kuna Hofmann, Sallman, na wengine wangapi zaidi, yote maelezo Yake mbalimbali, kwa hiyo ungechanganyikiwa kidogo jinsi angeonekana. Je! angeonekana kama alivyochorwa na Hofmann, ama Sallman, ama baadhi ya hao wengine? Hatujui. Kama Hofmann yu sahihi, basi Sallman amekosea. Mnaona? Sallman akiwa sahihi, basi Hofmann amekosea, na, mnaona, usingejua la kutafuta.

70 Lakini tungemtambuaje? Vema, tungemtambua jinsi vile Yeye alivyojitambulisha Mwenyewe hapo mwanzo, kweli, kwa kazi Zake, kwa yale aliyofanya. "Nisipozifanya kazi za Baba Yangu," Yeye alisema, "basi msiniamini Mimi. Lakini kama nikizitenda hizo kazi, ingawa hamuamini, aminini hizo kazi, kwa kuwa hizo ndizo zinazonishuhudia Mimi. Zinawaambia kile nilicho Mimi." Ingetubidi kutafuta basi, kwamba, kile kilichomfanya adhihirishwe. Kile kilichomtambulisha Yesu Kristo jana, kingekuwa ni kitu kile kile ambacho ingebidi kimtambulishe leo hii.

71 Sasa, sisi Wamethodisti tungewazia kanisa letu humtambulisha. Tungewazia hilo. Ninii yetu . . . Sisi Wabaptisti tungewazia kanisa letu lilimtambulisha. Na sisi Wapentekoste . . . Mnaona? Mimi ni hayo yote. Mnaona? Hilo, tungewazia. Tunafikiri kwamba letu lilimtambulisha.

72 Inanikumbusha, nilikuwa huko Little Rock, Arkansas. Huenda kukawa na baadhi ya marafiki zangu wazuri wa Arkansas hapa. Wao . . . Usiku mmoja, kwenye Chumba cha Mikutano cha Ukumbusho wa Robinson, kulikuwako na—na ombaomba aliyeketi barabarani, aliyekuwa na mikongojo, naye aliuza penseli. Naye alikuwa ameponywa. Basi kesho yake alikuwa akitembea kote, na mikongojo hii begani mwake, akishuhudia. Naye alikuwa huko juu kwenye roshani ya tatu, naye alikuwa tu akiteka ghorofa yote kule juu. Basi ilikuwa ni vigumu kwetu kuhubiri kwa sababu ya kelele. Naye alikuwa akipaza sauti na kupiga mayowe, aliishakuwa huku na huku mitaani, katika kila mahali pa biashara, akishuhudia, ameketi pembeni. Naye akaitwa, kwenye wasikilizaji, na Bwana Yesu akamponya.

73 Na kwa hiyo akasema, "Ninataka kukuuliza swali, Ndugu Branham."

Nikasema, "Ni nini, bwana?"

74 Akasema, "Unajua . . ." Yeye alikuwa ni Mnazarayo. Akasema, "Nilikusikia ukihubiri, na nikafikiri ulikuwa Mnazarayo." Kisha kasema, "Nikaona Wapentekoste wengi sana hapo, ndipo mtu fulani akaniambia ulikuwa Mpentekoste." Tena kasema, "Halafu nikasikia mtu fulani, aliyesema ya kwamba wewe ulikuwa ni mfuasi wa Kanisa la Baptisti ya Kimishenari." Kasema, "Vipi kuhusu hili?"

Nikasema, "Yote ni kweli. Mimi ni Mpentekoste Mnazarayo Baptisti."

75 Kwa hiyo, hilo, hilo—hilo ndilo. Mnaona? Tumezaliwa kwa Roho wa Mungu. Halafu, sisi ni ndugu na dada katika Kristo, nazo chapa hizi hazimaanishi chochote.

76 Nilikuwa nikiwachunga ng'ombe, na hapa juu, na mahali nilipofanya kazi kwenye ranchi, na—na huko Colorado. Nalo Shirika la Herefodi huchunga kwenye hilo bonde kule katika Mto Troublesome. Nasi tulikuwa na uzio wa kuhamishwa, na mahali wachungaji wanapoweka ng'ombe wao. Msimamizi anasimama pale, akiwahesabu hao ng'ombe wakati wanapopita. Nimesimama pale, mara nyingi, huku nimeweka mguu wangu juu ya ncha ya matandiko, nikiwaangalia hao wasimamizi. Sasa, kuna chapa za namna nyingi zinazopitia pale. Kila chapa kwenye hilo bonde hupitia pale. Msimamizi hakuwa akiangalia hizo chapa, bali alikuwa akiangalia kile kibandiko cha damu. Sasa, kibandiko hicho cha damu kilimaanisha ya kwamba ilibidi huyo awe ni Herefodi ukoo safi la sivyo asingeweza kulishwa kwenye hayo katika bonde hilo. Asingeweza kuingia bila kibandiko cha damu.

77 Nikawaza, siku moja, nikiwa nimeketi pale. Nilianza kupaza sauti. Nikasema, "Wajua, hivyo ndivyo itakavyokuwa kwenye ile Hukumu. Yeye hataangalia ni chapa gani waliyo nayo, bali kama tuna kibandiko cha Damu. Jambo ndilo hilo." Ata—atakapoiona hiyo Damu, basi tunaweza kuingia. Hivyo tu. Mnaona? Nazo chapa zetu zitakuwa zimesahaulika kwa mbali, wakati huo. Hiyo ni kweli. Nami nina furaha sana kwa ajili ya jambo hilo. Ni kweli. Sasa, nini . . .

78 Sasa, kama tunaweza kuona jinsi alivyojitambulisha Mwenyewe jana, basi tutajua kile atakachokuwa leo hii, kwa sababu angejitambulisha Mwenyewe yeye yule leo kama alivyokuwa jana. Hiyo ni kweli? Basi angefanya kazi za Mungu. Sasa, asingevalia . . .

79 Asingekuwa na elimu fulani. Hatuna kumbukumbu Yake kuenda shuleni. Na Yeye asingekuwa msemaji fulani wa kushawishi, kwa sababu tunaona ya kwamba lugha Yake ilikuwa mba—mbaya sana, hata, "Watu wa kawaida walimsikia kwa furaha." Mnaona? Kwa hiyo angekuwa tu ni Mtu.

80 Lakini kile ambacho kingemtambulisha kingekuwa utambulisho ambao Maandiko yanasema angekuwa. Na hivyo ndivyo ingetubidi kumtambua. Na hivyo ndivyo alivyotambulishwa wakati huo, kwa sababu hakuwa Mtu yeyote wa ajabu-ajabu katika madoido fulani ya mavazi. Hakuwa na dhehebu alilojivunia. Hakuwa na—na utambulisho kutoka kwa ushirika wowote ule, ambapo angeweza kusema, "Mimi ni mfuasi wa lililo kubwa zaidi ya yote." Ama . . . Mnaona? Yeye alikuwa tu na kazi za Mungu, ambazo zilikuwa zimethibitishwa na kunenwa habari zake, kwamba zingemtambulisha. Na huo ulikuwa ndio utambulisho Wake. Huo ulikuwa ndio Wake.

81 "Ni nani awezaye kunihukumu kwamba nina dhambi?" Na dhambi ni kutokuamini. Mnaona? "Ni nani kati yenu anayeweza kunihukumu? Ikiwa sijafanya yale hasa niliyopaswa kufanya, basi nyinyi niambieni mahali nimekosea," kwa maneno mengine. Mnaona? Sasa, hivyo ndivyo ingetambulishwa leo hii.

82 Sasa hebu tuone, basi, jinsi alivyotambulishwa katika siku hiyo. Je! ilikuwa ni kwa ushirika fulani? Ilikuwa ni kwa namna fulani ya elimu? Ilikuwa ni kwa alama fulani ya kisayansi aliyokuwa nayo? Ama ilikuwa ni kwa ushahidi wa Kimaandiko, ambapo alijitambulisha Mwenyewe, kwamba alikuwa ni Mwana wa Mungu? "Yachunguzeni Maandiko," Yeye alisema, "kwa kuwa Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi."

83 Maandiko ndiyo yanayomshuhudia Yeye. Kwa hiyo hayo ndiyo yaliyomtambulisha, yalikuwa ni Maandiko. Mnaamini hilo? Hayo ndiyo itabidi yamtambulishe leo hii, basi, ndipo tungejua kama tulikuwa sawa au la, kama ilikuwa ni Yeye. Yeye alikuwa ni yeye yule, angefanya vile vile. Sasa, hebu tuchukue sasa . . .

84 Tulisoma kutoka Yohana Mtakatifu, na hebu tulichukue tu kwa utulivu kwa dakika kumi ama kumi na tano zijazo, na kisha tuone kama Yeye atajitokeza na kuthibitisha Yeye ni Mungu, mnaona, tuone kama Yeye angali hai. Tunaamini ya kwamba Yeye hajafa. Hilo ni jambo moja . . .

85 Mimi ni mmishenari. Nimehubiri karibu katika kila taifa chini ya mbingu, kuzunguka mara saba. Nami nimeona kila namna ya dini, nikasimama mbele ya wachawi na kila dini potovu, nadhani, iliyopo, kadiri nijuavyo mimi. Na hata hivyo, kila moja yao, Budha, Islamu, Makalasinga, Wajaini, chochote iwezacho kuwa, zote zina mwanzilishi, na kila mwanzilishi amekufa. Wanaweza kutia alama kaburi lake, na huyo hapo amelala. Hiyo hapo mifupa yake.

86 Lakini, Ukristo, kuna kaburi tupu. Yeye yu hai. Na jambo zuri juu yake, sisi—sisi . . . Yeye anathibitisha kwamba yu hai. Yeye, Yeye yupo hapa sasa. Mnaona? Sasa, hilo ndilo jambo ambalo Mkristo anaweza kutulia juu yake, kwamba tunajua ya kwamba hayo makaburi mengine yote yamejaa. Lakini hili,

kuna kaburi tupu. "Hayuko hapa, bali Yeye amefufuka. Nasi tutawaambia ndugu habari hii njema." Naye yupo hapa, yeye yule jana, leo, na hata milele.

87 Sasa tutaanza na Yohana Mtakatifu, kwa kuwa tulisoma katika Yohana Mtakatifu. Na kila kitabu katika Biblia kitautangaza Ujumbe ule ule. Hakina budi kutangaza. Kama sivyo, si cha Kimaandiko.

88 Sasa tunaona, ya kwamba, wakati alipozaliwa. Hapa katika mlango wa kwanza wa Yohana Mtakatifu, tutaanzia kwenye mlango wa kwanza. Wakati Yeye alipozaliwa, tunajua kuzaliwa Kwake; na jinsi Malaika Gabrieli alivyokutangaza; na Mariamu mama Yake; na jinsi alivyochukuliwa mimba kwa Roho Mtakatifu. Na jinsi, kwenye umri wa miaka thelathini, alibatizwa na binamu yake, Yohana; ama binamu wa pili, Yohana Mbatizaji. Na mara akachukuliwa hata nyikani akajaribiwe, kwa siku arobaini, kisha akarudi katika nguvu za Roho. Katika nguvu za Roho Mtakatifu, Yeye alirudi kwenye huduma Yake.

89 Basi kumbukeni, Yeye aliwakataza wanafunzi kuhubiri tena, au kufanya lolote, mpaka walipoenda katika nguvu za Roho. Mnaona? "Ngojeni katika mji wa Yerusalemu hata mtakapovikwa nguvu kutoka Juu." Mnaona? Hampaswi kwenda mpaka itakapokuwa si ninyi, bali Mungu, watu wanaweza kuona uakisi wa Yesu Kristo ndani yenu. Ndipo watu wataamini, basi, kwa sababu haitakuwa ni nyinyi, itakuwa ni Yeye. "Na wote aliowajua tangu zamani, Yeye atawaita." Wataliona. "Kondoo wangu wanaijua Sauti Yangu." Sasa, tunaona kwamba, basi, mara tu wakati alipoingia katika huduma Yake.

Nitawataja watu wachache.

90 Ninawatakeni mkumbuke jambo moja. Kuna jamii tatu tu za watu duniani. Loo, tuna mataifa mengi, bali kuna tatu tu, na hizo ni kutoka kwa watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi. Hao walikuwa ni Myahudi, Mmataifa, na Msamaria. Tunaona, hapo Roho Mtakatifu alipotolewa, Petro alipewa funguo, akaufungua kwa—kwa Wayahudi kwenye Pentekoste, huko Yerusalemu; kwa Wasamaria; na pia kwa Wamataifa nyumbani mwa Kornelio, Matendo 10:49. Na tangu wakati huo umekuwa duniani kwa ajili ya jamii zote. Naye alikuwa na zile funguo, kuzifungulia jamii hizi.

91 Sasa, Wamataifa hawakuwa wakitarajia Masihi yeyote. Tulikuwa makafiri, sisi Anglo-Saksoni. Tulikuwa na marungu mgongoni mwetu na tuliabudu sanamu. Wala hatukuwa tukimtazamia Masihi yeyote. Bali Wayahudi walikuwa wakimtarajia Masihi. Nao Wasamaria, walikuwa wakimtazamia Masihi, ambao walikuwa ni nusu Myahudi na Mmataifa.

92 Sasa, tunajua ya kwamba Yeye huja tu na kujitambulisha Mwenyewe kwa wale wanaomtazamia. Na hivyo ndivyo itakavyokuwa katika Kuja Kwake kwa pili. Ulimwengu hautajua

chochote juu Yake. Yeye atakuja tu, alichukue Kanisa Lake na aondoke, nao wale ambao hawamtazamii wataachwa nyuma. Yeye anakuja tu kwa wale wanaomtazamia.

93 Sasa, Yeye alikuja kwa jamii yake mwenyewe, kwa Wayahudi. Sasa hebu tuangalie jinsi alivyojitambulisha Mwenyewe. Kitu cha kwanza tunachoona, kilikuwa ni Andrea hapa, na Filipo. Naye Andrea alikuwa amesikia habari za Yesu. Nao wakashuka wakaenda, kwa sababu walikuwa ni wanafunzi wa Yohana. Na walipoenda sasa. . . Nao walikuwa wamepata kazi Zake kuu, na wakaenda nyumbani pamoja na Yeye. Wakarudi kesho yake asubuhi, wameridhika kabisa ya kwamba huyo alikuwa ni Masihi.

94 Sasa tunaona ya kwamba Andrea anaenda na kumpata ndugu yake, Simoni, ambaye baadaye aliitwa Petro. Sasa, kama utasoma historia ya Simoni Petro, yeye na Andrea, walitoka katika nyumba ya kidini sana, Mafarisayo. Baba yao alikuwa mwaminio thabiti, mashuhuri. Naye alikuwa amemwambia mwanawe, "Sasa, wanangu, atakuja nanii . . . Sote tumekutazamia kote katika wakati kule kuja kwa Masihi, tangu ile ahadi yenyewe katika bustani ya Edeni. Ila sasa, kabla Yeye hajaja, kutakuwako na kuchanganyikiwa si haba, kwa sababu Shetani ataleta kila bandia anayoweza kuleta, mnaona, apate kukizuia kile Kitu halisi."

95 Sikuzote hufanya hivyo. Sikuzote hufanya hivyo. Lakini, kumbukeni, unapoona dola bandia, hapana budi pawe na dola halisi mahali fulani ambayo ilifanyiziwa. Ukimwona mtu akitekeleza sehemu ya mnafiki, kumbuka tu, kuna aliye halisi mahali fulani, ambaye anamwiga.

96 "Kwa hiyo, hapana shaka kwamba hilo lingetukia. Lakini," kasema, "sasa, wanangu, hili hapa mtakalokumbuka. Hatuna budi kuamini ujumbe wa Biblia. Naye Musa, mtumishi wetu, mtumishi wa Mungu ambaye alitupatia amri zetu na torati zetu, alisema ya kwamba Bwana Mungu wetu angemwinua nabii miongoni mwetu, mithili yake. Na sasa, Masihi atakapokuja, Biblia inasema ya kwamba Yeye atakuwa ni nabii. Nanyi mnajua ya kwamba tu—tumeambiwa ya kwamba tumpokee nabii tu baada ya yeye kutambulishwa na Mungu kwamba ni nabii."

97 Nanyi nyote wasomaji wa Biblia mnajua ya kwamba Neno la Bwana liliwajia manabii, hao tu. "Neno liliwajia manabii pekee." Na njia pekee ambayo mtu huyu angetambulishwa . . . Wamekaa miaka mia nne. Malaki angekuwa ndiye nabii wa mwisho.

98 Na sasa akasema, "Masihi huyu, wakati atakapokuja . . . Huenda wakainuka Masihi wa uongo. Huenda mambo ya kila namna yakatukia. Lakini Yeye atakapokuja, Mungu atamtambulisha. Atakuwa ni nabii. Biblia inasema Yeye atakuwa nabii. Nayo Biblia ilisema, 'Akiwepo mmoja miongoni

mwenu ambaye ni wa kiroho ama nabii, Mimi Bwana nitajitambulisha Mwenyewe kwake, nitasema naye kwa maono, na kadhalika. Na kama yale asemayo yakitimia, basi msikieni. Lakini yasipotimia, basi msimsikie.'"

99 Hilo ni aminifu na la haki kama tu . . . Hilo lina maana. Kama asemayo ni kweli, hayana budi kuwa kweli wakati wote. Huwezi tu kubahatisha hilo. Halina budi kuwa ni kweli. Kama ni kweli, haina budi kuwa ni Mungu. Na kama si kweli, basi si Mungu. Kwa hiyo hiyo ni ninii tu . . . Na kwa hiyo walijua kuamini hilo. Wayahudi wote walijua hilo, Wayahudi wa kweli.

100 Lakini, katika siku hiyo, kanisa lilikuwa na kitu kama lilicho nacho siku hizi, kidogo ni teketeke, na limeziendea kanuni za imani, na kuendea tabaka na matatizo ya ninii . . . na kuosha vyungu. Na kama Yesu alivyosema, "Mmeyachukua mapokeo yenu na kuzitangua Amri za Mungu juu yenu." Kwa mapokeo yao, hivyo ndivyo walikuwa wamefanya, zaidi sana kama leo hii, marudio ya wakati.

101 Sasa angalieni hili. Sasa, wakati Andrea aliporidhika kwamba huyo alikuwa Ndiye Masihi, Biblia haiweki tu kumbukumbu ya yale aliyofanya. Lakini alienda akampata Petro, ama jina lake lilikuwa ni Simoni wakati huo. Naye akasema, "Simoni, ninataka uje umsikie Mtu huyu. Yule nabii huko chini Yordani alisema Mtu huyu angekuja. Naye nabii alisema kwamba aliona Roho wa Mungu, kama hua, akija juu Yake. Naye alijua huyu alikuwa ni Mwana wa Mungu. Ninataka uje umsikie. Ipo Nuru, ishara, inayomfuata."

102 Kwa hiyo ningewazia Simoni alikuwa kidogo akisitasita kuja. Lakini, hatimaye, wakati alipotembea akaingia katika Uwepo wa Yesu . . . Sasa, litafakarini sasa, tunaenda kuangalia zile sifa, utambulisho, kile Yeye alichokuwa. Ndipo wakati . . . Ningali katika Yohana Mtakatifu, mlango wa kwanza. Basi wakati Yesu alipomwona Simoni akija Kwake, Yeye alisema, "Tazama Mwisraeli." Alinena, na alimfahamu. Akasema, "Jina lako ni Simoni. Wewe ni mwana wa Yona."

103 Hilo lilimwondolea ukakamavu. Alijuaje jina lake lilikuwa ni Simoni? Naye alimjuaje yule baba mzee mtauwa kabla yake, ambaye alikuwa amemfundisha ile njia? Alijua huyo hana budi kuwa ni Masihi. Ilikuwa ni nabii. Na mara akaanguka miguuni Pake. Pasipo na elimu, pasipo na ujuzi wowote—wowote nyuma yake, naye alikuwa amejiweka wakfu sana, hata Yesu Kristo akampa funguo za Ufalme, na kumfanya kiongozi wa kanisa huko Yerusalemu. Kwa kuwa punde tu ile . . . Yesu alijitambulisha Mwenyewe kwa kusema, "Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona," ambaye alikuwa ni baba yake. Hilo lilimfanya Yesu kuwa yule nabii kikamilifu. Petro aliliamini.

104 Sasa, tunaona kulikuwako na mmoja aliyesimama pale, jina lake Nathanaeli ama . . . Filipo, ninaamini ndivyo ilivyokuwa.

Filipo alikuwa amesimama hapo, naye akaona hili. Kwa hiyo, alikuwa Mwisraeli thabiti, naye alijua mahali palipokuwapo na ndugu ambaye walikuwa wamesoma pamoja. Sasa, kama umewahi kuwa Yerusalemu na kuona mahali Yesu alipokuwa akihubiria, na umbali ambao Filipo alilazimika kwenda, ni safari ya siku nzima kuizunguka milima, kufika mahali alipokuwa rafiki yake Nathanaeli, ambaye alikuwa ni mwanafunzi wa Biblia. Kwa hiyo akashika njia, mara moja, akiisha kuona kilicho Kweli. Alikuwa ameliona likifanya kazi. Aliridhika, huyo alikuwa ni Masihi.

105 Loo, laiti tungalikuwa tu na shauku hiyo, laiti tungeweza tu kupata kitu hicho hicho ndani yetu, wakati tunajua tumepata ile Lulu.

106 Huyo akauzunguka ule mlima. Hapana shaka kwamba alimpata Nathanaeli. Akaja nyumbani mwake, na—na labda akabisha mlangoni. Naye mke wake akasema, “Yuko—Yuko nje kwenye shamba la mizabibu.” Labda alilima mizeituni. Basi akatoka akaenda kwenye shamba la mizabibu. Naye akiwa Mkristo muungwana, hakumsumbua wakati alipokuwa akiomba.

107 Alikuwa amepiga magoti, akiomba. Labda alikuwa akiomba hivi, “Bwana Mungu, Yehova, ninazeeka. Nami nimetazamia na kutamani kumwona Masihi. Nijalie nimwone kabla sijaondoka.”

108 Na mara aliposema, “Amina,” na kuamka, ndipo Nathanaeli akasimama. Sasa, angalieni, si makelele mengi sana. Yeye alikuwa na—alikuwa na agizo.

109 Jambo ni kwamba, leo hii, tuna pitapita nyingi mno na kufanya mambo mengine. Basi hebu twende kwenye lengo. Je! Yeye ni Mungu ama Yeye si Mungu? Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, ama Yeye si yule yule? Yeye—Yeye angali ni Yesu? Amefufuka katika wafu? Ikiwa hajafufuka, basi sahau hilo. Ikiwa amefufuka, hebu tuamshe shauku zetu. Hebu na tujazwe na Roho Wake, tuanze kuomba na tuanzishe mkutano. Tufanye jambo fulani.

110 Angalia, yeye alienda moja kwa moja kwenye jambo muhimu, “Njoo, uone Yeye tuliyempata: Yesu wa Nazareti, Mwana wa Yusufu.”

111 Sasa, ningewazia mtu huyu mwenye imani halisi alipangusa mavazi ya—yake, kutokana na kupiga magoti kwenye mavumbi. Kasema, “Ngoja kidogo hapa, Filipo. Nimekujua kuwa mtu mwenye busara, bali huenda ikawa umeelekea kwenye ushupavu wa dini, wajua. Sasa, hapa, tunasoma Maandiko pamoja. Nasi tunajua ya kwamba. . . Ulisema nini, ati ‘Yesu wa Nazareti’? Sasa, unataka kuniambia ya kwamba Mwenyezi Mungu angeenda kwa kundi duni kama hilo kule chini Nazareti,” baya sana kuliko Tucson, “na kwenda kule chini, na,” ama Jeffersonville, ninakotoka, “huko chini kabisa kwenye mji huo

duni, na kuchukua kitu fulani huko chini? Mbona, unajua kuhani mkuu anaamini ya kwamba Yeye atashusha ushoroba kutoka Mbinguni, atembee moja kwa moja ugani, wajua. Nasi tumefundishwa hilo."

112 Lakini, mwajua, Yeye sikuzote haji jinsi tunavyofikiria huja. Mnaona? Yeye huja kwa unyenyekevu sana. Watu wameyapanga yote jinsi wanavyomtaka Yeye aje. Na sisi—sisi tunaupuuza unyenyekevu, na hapo ndipo unapompata Mungu. Wanasayansi leo hii wanaweza kumtuma mtu angani, katika mzingo, na kukanyaga jani ambalo hajui chochote kulihusu. Loo, inakubidi kujinyenyekeza, kumjua Mungu. Inakubidi kuyatupilia mbali mawazo yako mwenyewe, na kumfungulia tu moyo wako na maisha yako, ndipo atajitambulisha Mwenyewe.

113 Vema, ninaweza kumsikia akisema, "Chaweza kitu chochote chema kutoka Nazareti?"

114 "Yawezekana chochote kutoka kwenye hao watakatifu wanaojibingirisha, ama chochote unachotaka kuliita? Kama chochote kitafanyika, kitafanywa katika dhehebu langu, katika langu. Unaona? Hapo ndipo kingekuja. Mnaona? Yawezekana chochote chema kitoke kwenye kundi kama hilo?"

115 Sasa, nafikiri Filipo alimpa jibu zuri kuliko yote ambalo mtu yeyote angeweza kutoa. Alisema, "Njoo, uone."

116 Usikae nyumbani na kulikosoa. Njoo ujionee mwenyewe. Unaona? Unaona? Njoo uone. Ilete na Biblia yako na kulichunguza, uone kama ni kweli. Hivyo ndivyo kila mtu anavyopaswa kufanya. Mnaona? "Njoo, uone."

117 Hebu tuingilie mazungumzo yao wakati wakitembea ufukoni mwa Galilaya, wakija huku. Ninaweza kuwazia, kumsikia akisema hivi, "Hivi unamkumbuka yule mzee . . . Wajua, tumeninii—tumeizungumzia Biblia pamoja. Tumeketi pamoja katika ulimwengu wa roho, wakati tukiiangalia Biblia na kujua ya kwamba, siku moja. Sasa, Nathanaeli, nataka kukuuliza jambo fulani. Masihi atakuwa nini hapo atakapokuja? Tutajuaje kwamba Yeye ni Masihi?"

118 Mbona, Nathanaeli, akiwa mwanafunzi mzuri wa Biblia, alisema, "Mbona, Yeye atakuwa nabii. Hakika, Biblia ilisema Yeye angekuwa ni nabii. Vema, ndipo tutamjua."

119 "Je! unamfahamu yule mzee mvuvi asiye na elimu huko chini, ambaye ulinunua wale samaki kutoka kwake siku ile, naye hakuwa na elimu ya kutosha kutia sahihi risiti?"

"Naam, ninamkumbuka. Simoni, naam, mwana wa Yona."

120 "Wakati ndugu yake alipoenda akampata na kumleta mahali Yeye alipokuwa, Yeye alisimama na kumwangalia moja kwa moja usoni na kusema, 'Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.' Unajua, isingenishangaza, Nathanaeli, ila kwamba Yeye angesema, 'Jina lako ni Nathanaeli,' utakapofika pale. Unaona?"

121 "Aa, sina budi kuliona. Unajua, kuona ni kuamini," hata kutoka Missouri. Kwa hiyo tunaona, ya kwamba hapo walienda zao barabarani.

122 Basi mara Nathanaeli alipofika katika Uwepo wa Yesu Kristo, alifanya nini? Kulifanyika nini wakati alipofika mahali Yesu alipokuwa? Alisema, "Tazama Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake."

123 Vema, hilo hakika lilimwondoa majivuno mtu huyo. Naye akasema, "Rabi," ambalo linamaanisha *mwalimu*, "ulinijua lini Wewe? Sijawahi kukuona maishani mwangu. Ninaishi maili kumi na tano kuzunguka mlima hapa, na hata sijawahi kusikia habari Zako mpaka jana alasiri. Na hapa ninakuja kuzungukia huku na Wewe—na Wewe unaniambia kwamba mimi ni Mwisraeli."

124 Vema, unasema ni kwa sababu ya vile alivyokuwa amevalia. Loo, la. Watu wote wa Mashariki walivalia namna hiyo, na walifuga ndevu. "Wewe ni Mwisraeli ambaye ndani yake hamna hila." Sasa vipi kuhusu hilo?

Akasema, "Rabi, ulipata kuniona lini Wewe?"

125 Akasema, "Jana, ulipokuwa chini ya mti, kabla Filipo hajakuita, nalikuona." Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaona?

126 Alisema nini? Huenda kuhani wake alikuwa amesimama hapo. Huenda kulikuwako na wakosoaji wengi wamesimama hapo, ambapo walikuwako. Lakini yeye alimkimbilia, akasema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mfalme wa Israeli." Jina lake halifutiki usiku wa leo. Limeandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-kondoo.

127 Kulikuwako na wale waliosimama hapo karibu, hakika, ambao hawakuamini hilo. Hakika. Walisema, "Mtu huyu ni mpiga ramli. Yeye ni Beelizebuli." Ndipo Yesu akageuka. Kwa nini? Ilibidi watoe jibu kwa kusanyiko lao kwa ajili ya jambo fulani. Kazi zilikuwa zimefanywa. I—i—ilikuwa pale. Kwa hiyo akasema, "Mtu huyu ni Beelizebuli, mpiga ramli, mwana telepathia, ama kitu fulani."

128 Yesu akawaambia, "Ukisema hilo dhidi ya Mwana wa Adamu, utasamehewa. Bali siku moja Roho Mtakatifu yuaja, na kama ukisema . . . kufanya jambo lile lile. Na kama ukisema neno dhidi Yake, hutasamehewa kamwe, katika ulimwengu huu au katika ulimwengu ujao." Halitasamehewa kamwe. Sasa, hicho kilikuwa ni kizazi tunachoishi sasa.

129 Sasa tumekitambulisha kizazi cha kwanza. Tunaweza kuvileta vingine, lakini hebu twende sasa, maana itatulazimu kuanzisha mstari wa maombi. Walikuwepo Wayahudi, walio thabiti sana. Wakristo halisi, waaminio walioitwa na Mungu wanatambua hilo moja kwa moja.

130 Ndipo siku moja alikuwa akishuka kwenda Yeriko, bali alihitaji kupitia Samaria. Unashangaa ni kwa nini? Walikuwa wakimtazamia Masihi, bali sisi Wamataifa hatukuwa tukimtazamia.

131 Lakini sasa tunamtazamia Masihi. Unaona? Unaona, tumekuwa na miaka elfu mbili, kama walivyokuwa na miaka elfu mbili. Mnaona? Lakini tumekuwa na miaka elfu mbili, tukimtazamia. Tumesikia habari Zake, bali sasa tunamtazamia aje mara ya pili.

132 Na sasa tunaona ya kwamba Yeye alikuwa na haja kupanda kwenda Samaria. Hiyo ni huko juu mlimani. Basi alipopanda kwenda Samaria. Hapana shaka ilikuwa yapata adhuhuri, kwa hiyo akawatuma wanafunzi Wake mjini kununua maakuli. Kutoka mjini akaja maskini mwanamke mmoja.

133 Sasa, mkitaka, kama ningalikuwa na wakati, ningewafafanulia hilo na kuwaambia ni kwa nini alikuja majira hayo ya siku. Wanawake wote wenye tabia nzuri wanapaswa kuja pamoja. Wakaidi na wenye tabia nzuri hawashirikishwi pamoja. Hawawezi kuonekana hadharani, wakati ule ule, hata wa leo. Sasa, yeye alikuwa ametiwa alama, mwanamke mwenye sifa mbaya. Mnajua ninalozungumzia: kahaba.

134 Sasa, tunaona ya kwamba alikuja pale yapata saa tano mchana kuchukua, kuteka maji. Basi hebu tuwazie, yeye alikuwa ni mwanamke mrembo sana. Naye alikuwa amebeba chombo chake cha maji begani mwake. Nayo kidogo inatokea . . .

135 Nimewaona wakiweka mtungi mmoja juu ya kichwa chao, na mmoja kwenye kila nyonga, na kutembea, wakizungumza kama wanawake wawezavyo, na wasimwage hata tone moja. Na, hao, ni uwiano wa jinsi gani! Sijui jinsi wanavyofanya hilo. Lakini, hapa, akitembea, naye alikuwa na huu, una vipini viwili juu yake. Halafu wanaenda kisimani. Kina winchi, nawe unaishusha na kuchota maji, kisha unaivuta juu.

136 Na hiki kilikuwa ni kisima cha Yakobo, ambapo Yesu . . . Nje tu ya mji. Kilikuwa ni kisima cha umma. Na mahali ambapo Yakobo alikuwa amechimba kisima na kuwanywesha mifugo yake pale, na kwa hiyo alikuwa amekinywea, yeye mwenyewe.

137 Na kwa hiyo tunamwona mwanamke huyu akija kuteka maji yake, ndipo akaanza kushusha mtungi. Hebu tuwazie kwamba alikuwa akifikiria juu ya usiku uliotangulia. Basi akashusha, akaanza kushusha winchi, huku akifunga viopoo kwenye mi—mikono ya ile jagi, kuishusha chini ateke maji.

138 Ndipo akamsikia Mtu akisema, “Nipe maji ninywe.” Na ki—kisima pale, kama uliwahi kuwa kule, ni mandhari ndogo, kitu kama hiki hapa usiku wa leo. Na kuna mizabibu inayomelea ukutani. Na kwa hiyo Myahudi huyu alikuwa ameketi akiegemea ukuta.

139 Ndipo akatazama kule akaona Myahudi huyu ameketi pale ameegemea ukutani. Naye akasema, “Si kawaida kwenu Wayahudi kumwomba Msamaria chochote. Hatuchangamani sisi kwa sisi.” Vinginevyo, kulikuwa na ubaguzi. “Na hatuna uhusiano, mmoja na mwingine. Na Wewe ukiwa Mwanamume, na kuniomba mimi, mwanamke Msamaria, kukuletea maji unywe.”

140 Naye alikuwa Myahudi wa kawaida. Hakuvalia tofauti. Alikuwa Mwanamume. Nafikiri walisema, katika Yohana Mtakatifu 6, Yeye alikuwa na umri wa yapata miaka thelathini na miwili tu. Lakini alionekana, hapana shaka alionekana hamsini, maana wao walisema, “Wewe ni Mtu asiyepata bado zaidi ya miaka hamsini, na hata hivyo Wewe wasema ‘umemwona Ibrahimu.’”

Akasema, “Kabla Ibrahimu hajakuwako, MIMI NIKO.”

141 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] “ . . . usininii, usije hapa kuteka.” “Mbona,” akasema, “kisima ni kirefu, na Wewe una nini cha kufanyia? Unawezaje kuchota?”

142 Kasema, “Maji nitoayo ni maji kwenye nafsi.” Na mazungumzo yakaendelea. Sasa, yawabidi kuliamini Neno langu kwa hili, Yeye alikuwa akiwasiliana na roho yake. Mnaona?

143 Sasa, yeye alikuwa ni mwanamke, mwanamke mmoja kutoka Samaria. Kisha kasema, “Baba zetu walikinywea kisima hiki, na—na Wewe wasema una maji yaliyo makuu kuliko haya?” Naye akasema, “Na Wewe unasema, ‘Abuduni Yerusalemu,’ nao baba zetu waliabudu kwenye mlima huu,” na kadhalika.

144 Mazungumzo yakazidi kuendelea. Baada ya kitambo, wakati, Yeye akapata kile hasa shida yake ilikuwa. Ni wangapi wanajua shida yake ilikuwa ni nini? Hakika. Alipata mahali shida yake ilipokuwa. Akasema, “Nenda kamwite mume wako na mje hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

145 Sasa, kumbukeni, Yeye anafanya nini? Kujitambulisha Mwenyewe kwa Wasamaria sasa. Hivyo ndivyo alivyofanya kwa—kwa Wayahudi. Sasa, angalieni kile Msamaria huyu atakachosema.

Kasema, “Nenda kamwite mume wako na mje hapa.”

“Mbona,” akasema, “Sina mume.”

146 Akasema, “Umesema kweli, kusema ‘sina mume,’ kwa sababu umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako. Basi umesema kweli.”

147 Sasa mwangalie mwanamke huyo, huyo mwanamke Msamaria, jibu lake kwa hilo. Alijua mengi kuhusu Mungu kuliko nusu ya watu wa Marekani, mnaona, hakika, mnaona, pamoja na wahudumu, wakati mwingine. Naam. Mnaona?

148 Watazameni hao makuhani wamesimama pale. Walipoona hilo likifanywa, walisema, "Mtu huyu ni mpiga ramli. Yeye ni Beelizebuli," wakijaribu kuelewa jinsi alivyolifanya, vitimbi fulani, hila. Mnaona?

149 Bali maskini mwanamke huyu alisema, "Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii." Angalieni. "Tunajua, tunajua ya kwamba yuaja Masihi, aitwaye Kristo. Na atakapokuja, hivi ndivyo atakavyofanya." Amina.

Akasema, "Mimi ninayesema nawe, Ndiye."

150 Hilo lilitosha. Alijua huyo alikuwa ndiye. Angalia kile alichofanya. Akakurupuka kwenda mjini, naye akawaambia watu wa mjini, "Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo niliyotenda. Hii si ndiyo alama ya Masihi mwenyewe? Ni lini tumewahi kuwa nayo tangu wakati ule? Huyu hapa Masihi halisi."

151 Hivyo ndivyo Yeye alivyojitambulisha na Wayahudi. Hivyo ndivyo alivyojitambulisha Mwenyewe na Wasamaria. Sasa, huo ulikuwa ndio mwisho wa wakati wao.

152 Sasa, Mataifa wamekuwa na miaka elfu mbili ya mafundisho, kama hao walivyokuwa na maelfu ya miaka ya mafundisho. Lakini kama Mataifa hawatapata kitu kile kile walichopata, basi Yeye ana upendeleo. Kwa hiyo sisi tungemjuaje leo? Wakati aliposimama nasi, na ndani yetu, na kutenda kazi kupitia sisi, na kuthibitisha ya kwamba Roho huyu, ambaye tunamwita ubatizo wa Roho Mtakatifu, ni Yesu Kristo katika kujifanya Mwenyewe mwili katika mfano wa Roho katika mwanadamu, akifanya jambo lile lile. Yeye alisema katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 14, kifungu cha 12, "Yeye aaminiye," si anayejifanya kuamini. Bali, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye naye atazifanya." Hiyo si ni kweli?

153 Akasema, katika Yohana Mtakatifu 5:19. Alipitia kwenye birika la Bethesda. Ningali . . . Huo ni mlango wa 4 wa Yohana Mtakatifu. Sasa niko kwenye mlango wa 5. Katika mlango wa 5 wa Yohana Mtakatifu, Yeye alipitia kwenye birika la Bethesda. Hapo kulikuwako na umati mkubwa. Inahitaji elfu mbili kufanya umati mmoja. Kwa hiyo kuna umati wa watu katika hospitali hii kuu ya kiroho, tuseme, wamelala kwenye mlango wa kondoo wakingojea kutibuliwa kwa maji.

154 Mungu daima amekuwa na njia ya uponyaji wa Kiungu kwa ajili ya waaminio. Mnaona? Ndipo Malaika akashuka na kuyatibua maji. Yeyote wenu anajua maji yaliyotibuliwa ni nini, mnaona, ni mkondo ukienda upande mmoja, na upepo ukivumishia upande mwingine. Ni maji yaliyotibuliwa. Na ilikuwa ni huyo Malaika akija juu ya yale maji, akiyazungushazungusha. Ndipo wa kwanza kuingia ndani, kwa imani, alitoa nguvu kutoka kwenye hayo maji, naye akapona.

155 Yesu alipitia kwenye kundi hili la watu pale, na Yeye alijua mahali mtu fulani alikuwa amelala, ambaye alikuwa hawezi kwa miaka thelathini na minane. Labda alikuwa na ugonjwa wa tezi dume ama—ama kitu fulani. Haukuwa umuue. Ulikuwa umedumaa. Alikuwa nao, miaka thelathini na minane. Ndipo akamwendea, akasema, "Je! unataka kuwa mzima?"

156 Kwa nini hakusema hilo kwa viwete, vilema, vipofu, ama walioteseka? Walikuwa kule na watoto wenye vichwa vilivyojawa maji. Biblia ilisema, "Walikuwa viwete, vipofu, vilema."

157 Mtu huyu angeweza kutembea. Alisema, "Ninapokuwa nikishuka, mtu mwingine huenda mbele yangu." Lakini, kumbukeni, Yeye alijua mtu huyu alikuwa pale. Mnalipata?

158 Naye akasema, "Jitwike kitanda chako uende nyumbani mwako." Hamna swali kuhusu hilo. Akaenda zake, kwa kuwa Yeye alijua angefanya hivyo.

159 Wakamkuta amebeba kitanda chake, kwenye siku ya Sabato. Akaitwa ndani. Ingekuwa ni jambo lile lile usiku wa leo.

160 [Ndugu fulani anasema, "Ndugu Branham, ninataka Roho Mtakatifu."—Mh.] Kama—kama—kama mtu usiku wa leo. . . Mungu akubariki, ndugu, kumpokea.

161 Kama mtu usiku wa leo aliponywa, naye angeweza kuthibitisha, kwamba aliponywa, anajua ndani yake kwamba aliponywa, ugonjwa wa tezi dume, unafikiri nini kingetukia kesho? Mtu fulani angekuwa akisema, "Ninajua mtu fulani anayeketi pembeni. Ninajua mahali palipo na kiwete. Ninajua mahali *huyu* alipo, ama *yule* alipo. Nenda kawaponye." Mnaona, huyo ni ibilisi yule yule.

162 Yesu aliulizwa swali. Sikilizeni yale aliyosema katika Yohana Mtakatifu 5:19, "Amin, amin, nawaambia." Na *amin* linamaanisha, "Kabisa, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile amwonalo Baba analitenda. Hilo atenda Mwana vile vile." Mnaona? Yeye hakutenda lolote mpaka kwanza alipomwona Baba akimwonyesha hilo katika ono. Hilo lilimfanya Mungu-nabii.

163 Na leo hii Yeye angali ni yule yule, Mungu-Nabii yule yule, Roho Mtakatifu yule yule akiishi miongoni mwa watu. Tumempokea, katika mfano wa ubatizo. Tumempokea, katika kuombeana. Tumemwona akinena kwa lugha zingine. Tumemwona akizifasiri. Tumemwona akifanya ishara hizi kuu za siku hizi.

164 Na sasa tunapiga hatua kuingia katika jambo lingine. Tumekuwa na uigaji mwingi. Tulikuwa na mengi ya mambo haya, bali hilo haliliondoi kwenye Kweli ya Biblia. Yeye angali ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye angali ni Yesu Kristo. Yeye ni Mwana wa Mungu. Yeye yu hai milele.

165 Alisema, "Bado kitambo kidogo na ulimwengu . . ." Huo ni kosmosi, utaratibu wa ulimwengu, kundi la kawaida la kimadhehebu. "Hautaniona Mimi tena. Hata hivyo ninyi mtaniona, kwa kuwa Mimi . . ." Na "Mimi" ni kiwakilishi nafsi. "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata mwisho wa ulimwengu, hadi ukamilfu wa dahari. Mimi, Mimi Mwenyewe nitakuwa ndani yenu, nikifanya kazi Zangu zile zile nilizofanya, hata ukamilifu wa dahari, wakati wa mwisho." "Yeye yule jana, leo, na hata milele." Mungu tusaidie kuamini.

166 Sasa ningewaulizeni swali, kama Yeye ataonekana hapa miongoni mwetu usiku wa leo. Sasa, ninawatakeni mjue hili, ya kwamba hakuna kitu kama mponyaji wa Kiungu, si zaidi ya vile kulivyo na Mwokozi wa Kiungu duniani leo. Yeye yupo hapa katika umbo la Roho Mtakatifu, na Yeye yupo hapa tu kuthibitisha yale aliyoahidi tayari. Yeye yupo hapa, akilidhihirisha Neno Lake. Wakati alipokuja mara ya kwanza, Yeye alithibitisha ya kwamba alikuwa ni Masihi kwa yale aliyokuwa akifanya. Ilithibitisha ilikuwa ni Masihi.

167 Sasa, Yeye alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, na katika siku za Lutu." Katika siku za Nuhu, maji yalikuja. Katika siku za Lutu, moto ulishuka. Sisi tunatarajia nini kwa sasa? Moto. Tazameni jinsi alivyojithibitisha Mwenyewe.

168 Alishuka chini. Alikuwako Lutu, huko Sodoma, mfuasi vuguvugu wa kanisa, amerudi nyuma nusu. Pia kulikuwa na Malaika watatu walioshuka kutoka Mbinguni, nao wakamjia Ibrahimu kwanza, aliyewakilisha kundi lililoitwa litoke huko Sodoma, ambalo tayari limeitwa litoke.

169 Ndipo wawili wa hao Malaika wakashuka kwenda Sodoma na kuhubiri, hawakufanya miujiza mingi, Billy Graham mamboleo. Lakini alijitambulisha mwenyewe kama mtumishi wa Mungu. Ndipo mara Lutu alipotoka, mwenye uvuguvugu alipoondoka mjini, basi moto ukaangamiza mahali hapo.

Lakini ulitambua ni Mtu wa aina gani aliyekaa na Ibrahimu? Angalieni.

170 Sasa, Ibrahimu alikuwa na umri wa miaka mia moja, naye Sara alikuwa na tisini. Miaka ishirini na mitano, walikuwa wameamini ahadi hiyo ya mwana ajaye, wakiishikilia.

171 Hapo ndipo Yeye anapokuja, kwa wale wanaoamini, wakiishikilia ile ahadi.

Basi, tazameni, hao wawili walishuka kwenda kule.

172 Yule aliyekaa pamoja na Ibrahimu alijitambulisha Mwenyewe. Alikuwa ameketi ameelekeza mgongo Wake kwenye hema. Basi kumbukeni, yeye alikuwa "Abramu" mpaka siku moja au mbili tu kabla ya hapo, naye Sara alikuwa S-a-r-a-i. Sasa mke ni S-a-r-a na mume ni I-b-r-a-h-i-m-u, Ibrahimu. Basi mtazameni, Yeye alimwita (sio jina lake la kwanza) jina

lake alilopewa, siku moja au mbili hapo kabla. "Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?" S-a-r-a, binti mfalme.

Akasema, "Yuko hemani, nyuma Yako."

173 Sasa, Yeye alikuwa ameuelekeza mgongo Wake kwenye hema. Naye akasema, "Ibrahimu, Mimi, nitakuzuru," kulingana na ahadi aliyompa. Mnaona Yeye alikuwa ni Nani? Naye akasema, "Na Sara mkeo atamzaa mtoto huyu."

174 Naye Sara, katika hema nyuma Yake, Biblia inaonyesha mahali penyewe, "Alikuwa nyuma Yake, hemani. Akacheka moyoni mwake."

175 Naye Malaika akasema, "Kwa nini Sara akacheka?" Mnaona? "Kwa nini Sara akacheka?" Akijua yale aliyokuwa akifanya hemani, nyuma. Mnaona ninalomaanisha?

176 Ndipo Ibrahimu alipotoka nje, akamsindikiza, Yeye alienda Zake barabarani. Ibrahimu alisema ya kwamba alizungumza na Mungu, Elohimu. Nini? *Elohimu*, "Yule ajitoshelezaye kwa yote."

177 Ilikuwa ni ishara ya nini? Yesu alisema nini? "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Hiyo, hiyo . . .

178 Mtu fulani aliniambia, "Ndugu Branham, huamini huyo alikuwa ni Mungu, sivyo?" Biblia ilisema ilikuwa ni Mungu, na hayo ndiyo tu nijuayo. Alisema ilikuwa ni Mungu.

179 Ilikuwa ni ishara ya nini? Kwamba, Mungu, katika siku za mwisho, kabla ulimwengu haujaangamizwa, Yeye ataonekana katika kundi la walioitwa watoke, Mungu akijitambulisha Mwenyewe katika mwili wa binadamu miongoni mwa watu Wake. Huyu hapa, yeye yule jana, leo, na hata milele.

180 Sasa, si swali la kama Yeye atakuponya ama hatakuponya. Ni swali la kama Yeye yu hai ama si hai. Ikiwa Yeye yu hai, Yeye hutimiza ahadi Yake. Kama sivyo, ni hadithi tu ya kubuni ambayo tumesoma kutoka mahali fulani, na hayo ndiyo yote kwake. Ninaamini ya kwamba Yeye yu hai, usiku wa leo, miongoni mwetu. Mnaamini hilo?

181 Sina saa ya ukutani. Sioni . . . Saa yangu ya mkono imevunjika, na si—sijui ni saa ngapi. Kwa hiyo mtu fulani aniambie ni saa ngapi. [Mtu fulani anasema, "Saa nne kasorobo."—Mh.] Saa nne kasorobo. Niko ham- . . . Sasa hivi nimechelewa dakika arobaini na tano. Sikukusudia kufanya hivyo. Samahani. Mnisamehe.

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu.

182 Ninawaulizeni swali. Maandiko, majuma kadhaa tangu sasa, tungekuwa tukikaa kwenye somo lilo hilo. Ni utambulisho ya kwamba Yesu yupo hapa. "Mabwana, sisi tunataka kumwona Yesu." Basi, "Ni yule yule jana, leo, na hata milele." Kama mngeweza kumwona akiingia miongoni mwetu usiku wa leo na kufanya mambo yale yale tu papa hapa, aliyoyafanya

wakati alipotembea huko Galilaya, mngemwamini Yeye? Kama ungemwamini, inua mkono wako, useme, "Ningeamini kama ningaliweza tu kumwona akifanya jambo lile lile alilofanya kule."

183 Baba yetu wa Mbinguni, ni kundi la kupendeza sana la watu. Wanaitikia vizuri sana. Na mimi—mimi . . . Tuna furaha sana, wahudumu, Bwana, kuona watu wanaoitikia Injili. Inamaanisha ya kwamba kuna ishara, sauti ya upepo ukienda kasi hewani. Huenda ikawa ni kitu kile tulichoombea, hapa Tucson, kuona uamsho mkuu.

184 Tupo hapa kujitambulisha wenyewe kama watumishi Wako, kama shahidi wa kweli wa Biblia. Nasi tunajua, ya kwamba, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu." Nasi tunajua Biblia hii huonyesha mawazo ya Mungu kwa watu Wake. Nalo *Neno* ni "wazo lililotamkwa." Bwana, jalia tafakari lililoko moyoni mwangu, kwamba Wewe ni "yeye yule jana, leo, na hata milele," jalia Roho Mtakatifu asaidie usiku wa leo kulidhihirisha hilo Neno, ili liweze kuwa kweli iliyo hai moja kwa moja miongoni mwetu, tupate kuona ya kwamba Yesu yu hai.

185 Kwa kufanya hivyo, Bwana, ninaamini ya kwamba kusanyiko la watu litampokea. Wale ambao hawajaokoka watamtaka Mwokozi huyo wa ajabu. Kujua, ya kwamba, baada ya miaka elfu mbili, hii hapa ahadi Yake, ikiwa hai tu usiku wa leo kadiri ilivyokuwa ile saa aliyoifanya. Nao wagonjwa wataponywa; watakatifu watabarikiwa. Tunahisi ya kwamba uamsho tunaouombea utakuwa njiani. Bwana, hii ni kadiri mtu yeyote awezavyo kwenda, ni kusema tu yale Wewe umesema.

186 Sasa tunakutaka Wewe uje, mpendwa Yesu, na kutudhihirishia Uwepo Wako usiku wa leo, ili sote tuweze kujua ya kwamba Wewe upo hapa. Nalo litaisisimua mioyo yetu, Bwana, kujua, tunapotembea kuteremka barabarani. Itatufanya sisi sote kufikiria, wakati mwingine tutakapoanza kufanya lolote, ama kuwaza mambo mabaya, tujue ya kwamba Wewe unatuangalia. Tunajua ya kwamba Wewe upo hapa. Tunajua haiwezekani kabisa, Bwana, kwa hili kutendeka bila Wewe, kwa hiyo tunaomba ya kwamba Wewe utatujalia usiku wa leo. Katika Jina la Yesu. Amina.

187 Sasa, tunasambaza kadi za maombi kila siku. Na sasa, hatuwezi kuzichukua zote wakati mmoja. Pia tumechelewa kidogo. Ni—ninaamini ya kwamba tunapaswa kuufunga huu ifikapo saa nne. Basi tutaita tu kadi chache za maombi na kuwaombea wengine, wagonjwa, na labda Roho Mtakatifu atatujalia kitu miongoni mwetu.

188 Ninataka kila mtu aketi kwa utulivu kabisa. Iweni wanyamavu, watulivu tu mwezavyo kuwa. Shikilieni mahali

penu. Halafu basi, kumbukeni, ombeni.

189 Sasa, hebu tuone, tunaanzia mahali popote tu. Billy yuko mahali fulani hapa, laiti ningaliweza tu kuona mahali alipo. Alisambaza kadi za maombi. Sijui ni zipi alizosambaza. Loo, yuko nyuma kwenye kivuli, huko nyuma. Ati nini? A, moja mpaka mia moja. Vema. Hebu wanane ama kumi wasimame.

190 A, namba moja, ni nani aliye na kadi ya maombi A, namba moja? Kama huwezi kusimama, mbona, tutakubeba. Tutahakikisha kwamba wewe . . . A, namba moja? Hebu tuone, ni wapi? Afadhali uje *hivi*, nadhani. Ama, hivi? Vema. A, namba moja, tafadhali nenda moja kwa moja kule, mama. Baadhi . . .

191 A, namba mbili? Ni nani aliye na mbili, namba mbili? Ninajua ni Wahispaniola hapa. Namba mbili, waweza kuinua mkono wako ili tuweze kuona mahali ulipo? A, namba mbili. Muungwana mmoja kule nyuma. Tafadhali njoo hapa, bwana.

192 Namba tatu, namba tatu, aliye na kadi ya maombi tatu, waweza kuinua mkono wako juu? Mama. Naomba uje papa hapa, mama, tafadhali, tatu.

193 Nne, ni nani aliye na kadi ya maombi nne? Waweza kuinua mkono wako hapo? Muungwana huyu hapa, papa hapa. Vema.

Namba tano? Vema, *huku*.

Sita, ni nani aliye na kadi ya maombi sita, namba sita?

194 Mtu fulani aliseme katika Kihispaniola. Ati nini? [Ndugu mmoja anasema, "Seis."—Mh.] Seis? ["Seis."] Seis. Kadi ya maombi sita. Natumaini . . . Mnaona?

195 Angalia kadi ya maombi ya jirani yako. Huenda ikawa ni mtu aliye kiziwi. Hawawezi kukusikia, unaona. Wangekosa nafasi yao. Tunataka kila mtu aombewe. Kwa hiyo sasa angalia kama mtu yeyote, unashikilia kadi ya maombi, vema, sita. Huenda wakaninii . . .

196 Kuna zingine zilizoachwa hapa, dakika chache zilizopita, kwa hiyo huenda ikawa nilihubiri muda mrefu kupita kiasi, ama nilizungumza muda mrefu kupita kiasi, hasa. Ama, sikuhubiri, bali huenda wa—walichoka.

197 Sita, saba. Saba, waweza kuinua mkono wako? Saba. Nane, tisa. Hiyo ni sawa. Vema. Tisa, tisa, tisa, kadi ya maombi tisa? Ni mvulana mdogo? Una kadi ya maombi tisa, mwanangu? Nane. Vema. Hilo ni sawa. Namba nane, tisa?

198 Sasa, mnapopata kadi za maombi, tazameni, msi—msi—msizichukue tu, mnaona, na—na usije huku, kwa sababu unamnyang'anya mtu fulani mahali hapo, unaona. Nawe, huna budi kuja na kuchukua kadi yako mwenyewe ya maombi. Unaona, mtu fulani akija na kuchukua moja, ampe mtu mwingine, kisha wanaamka na kutoka nje, halafu basi, mnaona, mtu fulani anapakosa mahali hapo ambapo mtu fulani angaliingilia. Vema.

199 Kuna sita na tisa ambazo ziko nje. Ni nani anayeweza kusema katika Kihispaniola, kwa sauti kubwa kabisa? [Mtu fulani anasema, “Nueve.”—Mh.] Vema. Chochote kile hilo lilichokuwa, vema, hilo ni sawa. Vema. Kama kadi hiyo ya maombi iko hapa, vema.

200 Je, mama huyo ana hiyo, sita ama tisa? Wewe, sita? Sawa. Vema.

201 Tisa, sasa, ni nani aliye na kadi ya maombi tisa? [Mtu fulani anasema, “Waliondoka.”—Mh.] Waliondoka. Vema. Vema.

202 Hebu tuanzie hapa, basi. Vema, tuanzishe mstari wa maombi, na kuanza.

203 Sasa, halafu basi, tu—tumeharakisha kidogo, kwa hiyo msiwe na wasiwasi sasa. Tutaondoka katika dakika kumi, kumi na tano. Lakini ninataka kuwaulizeni jambo fulani.

204 Ndilo hilo, ndugu zangu. Sasa laiti mngalininii, nafasi kidogo tu hapo, mki—mkiweza. Asanteni.

205 [Ndugu mmoja anasema, “Ndugu Branham, si lazima tuwe tumetoka hapa ifikapo saa nne. Chukua wakati wako.”—Mh.] Ndugu ndio kwanza aje, akaniambia, si lazima tuwe tumetoka hapa ifikapo saa nne. Kwa hiyo, hilo ni sawa. Vema, hatutaki kuwachosha watu.

206 Jambo ndilo—jambo ndilo hili hapa. Kadiri niwezavyo kuona . . . Sasa, ni wangapi huko nje wasio na kadi za maombi, na hata hivyo wewe ni mgonjwa? Inua mkono wako, hamna kadi za maombi. Loo, ni kila mahali tu. Sio lazima uwe na kadi ya maombi. Inakubidi uwe na imani. Mnaona? Kadi ya maombi ni kitu tu unachoshikilia mkononi mwako. Unaona? Wewe . . . Ni kadi tu iliyo na namba juu yake. Ni hayo tu, kadi yenye namba moja, mbili, tatu, ama chochote ilicho. Na wakati mwingine sisi . . . Kila siku tunasambaza kadi mpya, maana kuna watu wanaokuja. Ndipo tunaanzia mahali pamoja, na pengine. Hakika.

207 Ni wangapi waliowahi kuwa katika mmoja wa mikutano hapo awali? Hebu tuone mkono wako. Loo, loo, nilifikiri nilikuwa mbele ya kusanyiko geni, na halafu kuzungumza juu ya jambo kama hilo. Mnaona? Mbona, la. Kuna theluthi mbili hapa ndani wamekuwa katika mikutano hapo kabla. Vema. Mnaelewa lile, jinsi tunavyolifanya.

208 Sasa, sioni mtu kwenye wakati huu ambaye ningeweza kusema ninamjua. Hu—huenda nikajua baadhi yenu, bali hakuna mmoja ninayemwona ambaye ninamjua. Siwezi kumwona mtu mmoja.

209 Ni—ninajua mke wangu yuko hapa ndani mahali fulani, na mmoja wa binti zangu, lakini, na, lakini, hata sijui mahali alipo. Yuko hapa ndani mahali fulani. Lakini si—sijui . . .

210 Na ninajua ya kwamba nilimsikia Ndugu Fred Sothmann, mmoja wa wadhamini wetu wa kanisa huko Indiana, akisema, "Amina," muda mfupi uliopita. Lakini Baba Yangu wa Mbinguni anajua siwezi hata kumwona mtu huyo. Kidogo ni vigumu kuona kutoka hapa. Hata sijui mahali alipo.

Sioni yeyote nimjuaye, hata mmoja wenu.

211 Lakini, na wote walio kwenye mstari huu wa maombi, ninyi mlio kwenye mstari wa maombi, ninyi nyote msionijua mimi, ama unajua ya kwamba mimi sikujui, inua mkono wako, kwamba unajua. Vema. Kundi lote lao. Siwajui. Hawanijui. Hamnijui, na mimi siwajui.

212 Sasa, jambo lenyewe sasa ni kwamba, je! Yesu Kristo yu hai? Hilo ndilo tunalotaka kujua. Mnaona? Na sasa hata hatuwezi. . . Yapo mambo mengi ambayo tungeweza kusema. "Naam, ninamhisi moyoni mwangu."

213 Watu wanasema, "Jambo lingine." Nao wanasema mambo mengi. Wanasema, "Hiyo ni saikolojia."

214 Lakini tunataka kujua, je! Yeye yu hai kweli, kujitambulisha Mwenyewe Kimaandiko kuwa yeye yule jana, leo, na hata milele? Hilo ndilo tunalotaka kujua.

215 Sasa, hili hapa Neno la Mungu, nami ninalishika mkononi mwangu. Hakuna mtu ninayeweza kumwona, ukiacha mwanangu sasa.

216 Na Ndugu Tony anayeketi hapa chini, ila rais wa Ushirika wa Wafanyabiashara wa Full Gospel, ndio watu wawili pekee ninaowaona, ambao ninawajua.

217 Maskini wale waimbaji wanaoketi pale mwishoni, na—nafikiri ni wazuri sana. Ninaamini huyu ndiye mama yao anayeketi papa hapa. Sina hakika. Ama—ama, hiyo ni kweli? Nimekosea juu ya hilo? Vema, nimekosea hapo. Kwa hiyo, si—sijui. Nimemwona mama fulani akicheza. Ndiye huyu kwenye piano? Vema, nilimwona mama, hivi majuzi usiku, akicheza pale juu, aliyefanana sana na mama huyu hapa, ambaye nilidhani ndi—ndiye mama yake. Wa nanii—wa nanii. . . Yule pale. Naam, bwana. Hiyo ni kweli. Vema, sasa, itakubidi kusema, wanafanana sana. Hiyo ni kweli. Lakini, hiyo, mnaona, hata sikumjua mama huyo.

218 Sasa, hivyo basi, nimesimama hapa pamoja na wahudumu walionizunguka, nyuma yangu, na huko mbele, Wakristo. Basi hapa tumesimama hapa. Nami nadai ya kwamba ushahidi wa Biblia wa Yesu Kristo ni ishara ya kinabii. Biblia inasema hivyo. Na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Na aliahidi ya kwamba, kama tukimwamini Yeye, kazi alizofanya Yeye sisi nasi tungezifanya. Sasa, hiyo ni kweli?

219 Sasa, kama hiyo ni kweli, kila mwenye dhambi anapaswa kujikuta hapa madhabahuni, mahali hapa, na kuomba msamaha

wa dhambi. Kila mgonjwa anapaswa kuukubali uponyaji wako papo hapo ulipo.

220 Kwa sababu, hakuna nguvu ndani yangu. Mimi ni mwanadamu. Huyu hapa mchungaji wenu, ni kama tu nilivyo mimi. Sisi ni watumishi tu wa Kristo. Lakini, tupo hapa. Sasa, wao ni—wao ni wahubiri. Mimi si mhubiri sana. Mnajua hilo, kufikia sasa. Lakini ni—ni. . .Hao ni wahudumu, walimu, na kadhalika. Mimi si mhudumu, au mhubiri, hasa, kwa sababu sina elimu, ama, wala kisomo. Pia sina digrii za. . .na ninii. . . Sina ma B.A. wala ma D.D, wala. . .ni—ni kwamba tu sina. Na mimi—mimi—mimi. . .Ila Bwana alinipa ka—karama, kwa sababu ninampenda. Na Yeye—Yeye hunijalia kumfanyia kazi kwa njia hii.

221 Na kama atajidhihirisha Mwenyewe hapa; kwamba Yeye yupo hapa; na Roho Mtakatifu yuyu huyu mnayempokea, anathibitisha kwamba ni Yeye. Pentekoste ndicho kitu pekee kitakachouthibitisha Ukristo. Huwezi kuuthibitisha kwa sayansi. Huwezi kuuthibitisha kwa kitu chochote ila kwa ujuzi wa kipentekoste. Ninyi Wabaptisti mnajua hilo, na nyinyi Wamethodisti na Wapresbiteri, na chochote mlicho.

Mnajua inahitaji ujuzi wa kipentekoste kumthibitisha Mungu. Na hilo ni kwa kila mtu binafsi. Haithibitishi dhehebu. Inamthibitisha mtu binafsi.

222 Kama vile Yesu alivyomwambia Petro, wakati aliposema, "Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu." Alisema, "Mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni. Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kamwe kulivunjilia mbali, mnaona, hayawezi kulishinda."

Sasa, iko wapi? Mama huyu.

223 Sasa, kama Yesu Kristo akithibitisha kwamba Yeye yu hai, ni wangapi watakaoukubali uponyaji wenu, papo hapo mnapoketi? Inua tu mkono wako, useme, "Kama Yeye atafanya yale tu aliyofanya hapa, ninajua Yeye yu hai. Ndugu Branham, ni—nilikusikia ukizungumza. Ninakujua. Wewe ni maskini mhubiri mwenye upara tu anayesimama hapo, unaona, nami ninajua hakuna chochote ndani yako. Lakini ni—ninajua, kama umesema Kweli, Mungu bila shaka ataishuhudia. Anawajibika kufanya hivyo."

224 Sasa, nimenena habari Zake. Sasa hebu Yeye anene, kwamba nimewaambia Kweli. Kama si Kweli, basi si Kweli. Kama ni Kweli, basi ikubalini.

225 Mama huyu hapa, sijawahi kumwona. Aliinua mikono yake, dakika chache zilizopita, kwamba tulikuwa hatufahamiani. Huenda alisikia habari zangu mahali fulani, kwenye gazeti la kila siku, jarida, ama huenda aliniona mkutanoni. Lakini kuhusu kujua lolote juu ya mwanamke huyu, la kwanza,

jambo pekee nijualo, labda kamwe sijakutana naye hapo awali maishani. Amesimama hapa, mgeni kabisa.

226 Aisee, hili limetokea kuwa ni jambo nililozungumzia, dakika chache zilizopita. Huyu hapa mwanamume na mwanamke, wanakutana kwa mara ya kwanza, kama vile Yohana Mtakatifu mlango wa 4, wakati Bwana wetu Yesu Kristo alipokutana na yule mwanamke kisimani. Moja kwa moja kwenye mandhari, vile vile, ni Biblia tu ikionyeshwa tena. Yesu kamwe hakumjua. Yeye kamwe hakumjua Yesu. Mwanamke alimpa swali, akimwuliza, na—na Yeye akamwomba maji anywe. Halafu basi Baba alipomfunulia kilichokuwa shida ya mwanamke huyo, upesi akatambua ya kwamba huyo alikuwa ni zaidi ya mtu tu wa kawaida.

227 Sasa, mama, si—sikujui, sijui jambo moja kukuhusu. Lakini ninazungumza nawe tu, ama wewe ukiwa ndiwe mtu wa kwanza kumshika Roho wa Bwana. Na sasa naona kwamba wewe ni mwaminio, na ninamaanisha Mkristo mwaminio, sio mwomba lifti. Kwa sababu, mara, nilipokugeukia, roho yako inadundadunda kwa makaribisho. Unaona, ninajua ya kwamba yeye ni Mkristo. Mnaona? Sasa, angeweza kuwa ni mnafiki; angeweza kuwa chochote; angeweza kuwa ni mdanganyifu anayesimama hapo. Ningejuaje? Sijawahi kumwona maishani mwangu.

228 Lakini, sasa, kama—kama hili likijirudia, kwamba Yeye anajua mahali shida yako ilipo, anajua sababu ya wewe kuwa hapa. Huenda ikawa ni maradhi. Huenda ikawa ni matatizo ya kifedha. Huenda ikawa ni matatizo ya kinyumbani. Sijui mimi. Yeye anajua. Lakini iwapo atanifunulia mimi kwa Uwepo Wake, na ajalie nia yangu na midomo, na yote, ibebwe sana na Yeye, hata Yeye akwambie kilichokuleta hapa. Unajua kama ni kweli ama si kweli, sivyo? Ungejua, kama ilikuwa ni kweli ama si kweli.

Ni wangapi wangeliliamini? Mnaona?

229 Sasa, mimi hapa, huku mikono yangu imeinuliwa juu, pia. Sijawahi kumwona maishani mwangu, kama nijuavyo mimi. Sijawahi kumwona maishani mwangu. Hatufahamiani kabisa, mmoja kwa mwingine. Sasa, kama Roho Mtakatifu anaweza kufunua, kwa mwanamke huyu, jambo fulani kumhusu: jambo fulani alilofanya, kama mwanamke yule alivyofanya kisimani wakati ule; ama jambo fulani alilopaswa kufanya, na hakulifanya; tatizo fulani ambalo amekuwa nalo; kitu kilicho moyoni mwake; kitu anachotaka, au kitu kama hicho; hakina budi kutoka kwa Nguvu fulani za kimbinguni. Ni wangapi wanajua hilo?

230 Vema, sasa, ungeweza kuchukua upande wa Mafarisayo, na kusema, “Ni ibilisi.” Ama, ungeweza kuchukua upande wa

mwaminio, na kusema, “Ni Mungu.” Basi, inakutegemea wewe. Ni juu yako.

Sasa, hilo, Roho Mtakatifu na anene.

231 Sasa, kama ninyi ambao mnazidhibiti maikrofoni hizi, mara nyingine wakati Upako unaposhuka, ambapo si—sijui ninazungumza kwa sauti kubwa jinsi gani.

232 Mnaona mahali inaponibidi kusimama sasa? Ama inanibidi kusimama pamoja na Neno hili . . . Nami nimetangaza kwamba Hilo ni Kweli. Sasa sina budi kumtegemea Mungu kulijibu hilo wazi, kwamba ni Kweli, papa hapa mbele ya watu hawa.

233 Nilifanya hili mbele ya nusu milioni. Mungu alilifanya hilo, hasa, hebu niseme, huko Bombay, India, mbele ya mia mbili na hamsini elfu.

234 Huko Afrika Kusini, kwenye uwanja wa mbio za farasi, wakati wenyeji elfu thelathini wanaovaa blanketi walipompokea Kristo. Na elfu ishirini na tano, waliolala kwenye machela na kila kitu, walisimama na kwenda zao, wakati uo huo. Hao walikuwa—hao walikuwa waabudu sanamu.

235 Inapaswa kufanya nini kwa kundi lililozaliwa mara ya pili linalomwamini Mungu na linalotazamia kitu kama hicho kutukia? Miujiza elfu ishirini na tano kufanyika tu kwa wakati mmoja, hilo tu ndilo walilotaka kuona, punde tu lilipotendeka. Linapaswa kutufanyia nini sisi?

236 Sasa, dada yangu, sisi ni watu wawili, tuliozaliwa katika sehemu mbalimbali za ulimwengu, labda, na kukutana kwa mara yetu ya kwanza hapa sasa. Nami ni—ninataka tu kuzungumza na wewe, kusudi, kama Yeye atanifunulia mimi, huku sisi sote tukingojea kuona ni nini kinachotukia. Sasa, haina budi kuwa ni Yeye, kwa sababu si—sikujui mimi. Sijawahi kukuona, lakini Mungu anakujua.

237 Lakini sasa kama kusanyiko . . . Ni nani aliyewahi kuiona ile Nuru, ile picha ya Malaika wa Bwana? Ni wangapi wamewahi kuiona Hiyo? Mnaona? Vema. Hii hapa, papa hapa kati yangu na mwanamke huyu, sasa hivi. Hamwezi kuiona Hiyo? Inasongea kwake. Mnaiona Hiyo? Mnaona? Huyu mwanamke anaiangalia, yeye mwenyewe.

238 Mwanamke huyu ana matatizo. Anayo mambo mengi kasoro. Moja ya shida zake kubwa ni ugonjwa wa kibofu nyongo. Hiyo ni kweli. Sasa, kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

239 Sasa mnaamini? Na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Sivyo? Mnaamini hilo, ndugu?

240 Ninaendelea kuhisi hiyo ikija, mtu fulani alisema, “Alibahatisha hilo.” Sikubahatisha hilo. Basi, mnaona, huwezi kujificha sasa. Roho Mtakatifu yupo hapa. Unalowaza, nitalishika. Yesu alijua mawazo yao, mnaona. Na mimi si Yesu, lakini Yeye yupo hapa pamoja nasi. Mnaona?

241 Hapa, sikujui. Naye Yesu ataniambia kwamba wewe ni nani, basi hilo linapaswa kuliondoa swali kwake, kwa wakati wote. Sivyo? Bibi Heineman, nenda zako. Umeponywa. Yesu Kristo anakupa afya. Amina. Amina.

Mnaamini sasa? Unasema, “Ati jina la mwanamke huyo?”

242 Kwa nini, hivi hakumwambia Simoni jina lake lilikuwa ni nani, baba yake alikuwa ni nani? Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaamini hilo?

243 U hali gani, bwana? Huyu hapa mwanamume ambaye sijawahi kumwona maishani mwangu. Nadhani hatufahamiani, mmoja kwa mwingine. Hiyo ni kweli. Ili watu wajue, inua tu mkono wako ili watu waweze kuona kwamba hatufahamiani. Sijawahi kumwona mtu huyu. Anaonekana kana kwamba a— ana afya kutosha. Simjui mtu huyu. Sijawahi kumwona. Mungu anajua yote kumhusu.

244 Sasa, kama alikuwa mgonjwa na ningeweza kumponya, si ningekuwa mtu mbaya sana kama sikumponya?

245 Bali nisingeweza kumponya, kwa sababu siwezi kufanya kile Kristo amefanya tayari. Ameponywa tayari, kama yeye ni mgonjwa. Ni kitu fulani tu cha. . . Kama Yesu alikuwa amesimama papa hapa amevaa suti hii, ambayo Yeye alinipa, asingeweza kukuponya. Angekwambia alikuwa amefanya hivyo tayari. Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake. Angekuuliza kama unaamini hilo.

246 Lakini angeweza kujitambulisha Mwenyewe ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, na hivyo ndivyo tu Yeye anavyofanya. Mnaona? Hiyo ni kweli.

247 Sasa, huyu hapa mwanamume. Yule mwingine alikuwa ni mwanamke. Sijawahi kumwona, kukutana naye. Sisi ni wageni tu hapa duniani. Sasa, bwana, kama Roho Mtakatifu mkuu. . .

248 Ambaye, unajua sasa hivi, kitu fulani kilitukia wakati uo huo basi. Sivyo? Sasa, Nuru hiyo ilikaa moja kwa moja juu ya mtu huyu. Mwulizeni tu. Ninakutaka ujue hili. Yapata sekunde moja tu iliyopita, hisi tamu nyenyekevu kwelikweli ilikuja juu yako. Hiyo ni kweli? Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Mnaona? Ninaiangalia Hiyo moja kwa moja, mnaona, pale. Vema.

249 Mtu huyu anasikia kwa shida sana katika masikio yake, bali amekuwa na tukio baya sana lililompata. Amekuwa na upasuaji kwa ajili ya ngiri. Hilo ndilo unalotaka niombee. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema.

250 Hiyo ni kweli? Mnaamini hilo?

Sasa, unaona, huyabahatishi mambo hayo. Ni ya kweli.

251 Hapa, ana kitu fulani moyoni mwake, unataka kuamini kama ni Mungu ama siye. Kuna kitu kingine moyoni mwako, kitu fulani unachotaka. Kuna mtu fulani nje hapa kwenye wasikilizaji, anayeteseka, pia. Ni mke wako. Hiyo ni kweli. Ana

matatizo, katika mateso na maumivu, sasa hivi. Hiyo si ni kweli? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Vema, dada, umeponywa, pia. Nyote wawili nendeni nyumbani. Yesu Kristo anakufanya mzima. Nenda zako, ukishangilia. Mshukuru Mungu. Uponywe. Ubarikiwe!

252 Aminini sasa. Iweni na imani. Msitie shaka. Aminini. Mambo yote yanawezekana kwao waaminio. Mnaona? Siwezi kuponya. Mimi si mponyaji. Lakini Yesu Kristo anajithibitisha Mwenyewe ya kwamba yupo hapa pamoja nanyi.

253 Huyu, kwa namna fulani ni mama Mhindi ama Mmeksiko anayeniangalia, papa hapa, akiugua shinikizo kuu la damu. Unamwamini Yesu Kristo? Sikujui. Sijawahi kukuona. Hiyo ni kweli? Lakini, ulikuwa umeketi pale, ulikuwa ukiamini hilo. Sivyo? Simama kwa miguu yako, kama hiyo ni kweli, kama unaugua shinikizo kuu la damu. Yesu Kristo alikuponya.

254 Ni kitu gani kilichotokea hapo? Unasema, "Ndugu Branham, hayo si Maandiko." Naam, ni Maandiko. Mwanamke aligusa vazi Lake. Hiyo ni kweli?

255 Sasa, ni wangapi wenu ninyi wahudumu na ninyi watu mnaamini hili, kwamba Biblia inasema, ya kwamba, "Yeye sasa ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu?" Hiyo ni kweli? Ungejuaje kwamba ulimgusa? Kwa sababu alitenda sawa na alivyotenda jana. Amina. Inamfanya yeye yule jana, leo, na hata milele.

Maskini mwanamke yule mdogo anayeketi pale, mnaona, imani yake!

256 Kulikuwa na mwanamke wakati mmoja aliyepitia kwenye umati wa watu, naye akaligusa vazi Lake, kwa maana alisema ndani yake mwenyewe, "Ninaamini ya kwamba Mtu huyu ni mkweli. Ninaamini Yeye ni Mwana wa Mungu. Na kama ninaweza tu kugusa upindo wa vazi Lake, nitapata kupona, afya." Ni wangapi wanaijua hadithi hiyo? Vema, basi, ikiwa Yeye . . .

257 Biblia inasema, katika Agano Jipya, kitabu cha Waebrania, ya kwamba, "Yeye ni Kuhani Mkuu ambaye sasa hivi anaweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu." Tunajuaje tulimgusa? Kwa sababu Yeye anatenda vile vile alivyofanya jana.

258 Sasa, mnajua mwanamke huyo kamwe hakunigusa mimi. Yuko futi thelathini kutoka kwangu.

259 Bali alimgusa Yule Kuhani Mkuu tunayewasiliana naye. Haya basi. Kila mmoja wenu anaweza kufanya hivyo kama tu utaamini. Amina. Mnaona Yeye ni yule yule?

260 Sasa mwulizeni maskini mwanamke huyo. Sijawahi kumwona, kamwe sikumjua. Yeye ni mwanamke tu aliyeketi hapo.

261 Samahani. Hatufahamiani, sisi kwa sisi, bali Yesu Kristo anatujua sote wawili. Unaamini ya kwamba Yeye anaweza kunifunulia mimi jambo fulani ulilotenda, jambo fulani unalotamani? Ingekufanya ujue hilo? Mimi, ndugu yako tu, nisingejua hilo. Itabidi litoke kwenye mamlaka fulani. Ungeamini kuwa ni Yesu Kristo? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Ungeamini. Ninaamini ungeamini, maana wewe ni Mkristo. Vema. Wewe, niamini mimi sasa.

262 Na sasa je! kusanyiko litaamini kwa moyo wao wote? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaamini ya kwamba saa tunayoishi, kwamba mambo haya yanapaswa kuja sasa hivi? ["Amina."] Kumbukeni, hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho ambayo Israeli walikuwa nayo kabla hawajaninii . . . "Waliochukuliwa, walichukuliwa. Walioachwa, waliachwa." Hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho kabla moto kushuka. Hiyo ni kweli?

263 Tumekuwa na ishara, maajabu, utakaso, ubatizo wa Roho Mtakatifu, kunena kwa lugha, uponyaji wa Kiungu. Lakini ni nini kilichokuwa ishara ya mwisho kabla ya Sodoma kuteketezwa? Kitu hiki hiki mnachokiona usiku wa leo, Mungu akijidhihirisha Mwenyewe katika mwili wa mwanadamu, akijua siri ya moyo. Yesu Kristo alisema hivyo. "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu."

264 "Aisee, unamwangalia mwanamke huyo. Unasoma akili yake." Nitampa kisogo basi. Mnaona? Msidhani sishiki mnayowazia, maana ninayashika. Vema.

265 Mama, ndio kwanza uje hapa sasa, kwa hiyo nitaangalia juu na nisimshike mtu mwingine. Sasa, hatufahamiani kabisa. Lakini iwapo Yesu Kristo anaweza kunifunulia kilicho shida yako, utaamini? Kama utaamini, inua mkono wako.

266 Ninaona wewe una wasiwasi kupindukia. Hiyo ni kweli. Na sana sana hilo hutokea karibu mwisho wa alasiri, unapochoka na kudhoofika, kila kitu huonekana kinakuwa ni cha kigeni kwako. Unaugua pia baridi yabisi. Hiyo ni kweli. Punga mkono wako. Naam. Na nimeona kwamba wakati unaponinii—wakati unapojaribu kutoka kitandani, unaenda polepole sana, unapoamka asubuhi. Kidogo ni vigumu kwako wakati huo. Hiyo ni kweli.

267 Jambo fulani la kigeni. Ninaona mtu, mvulana, akijitokeza hapa. Ni mwanao, naye anaugua ugonjwa wa akili. Na ugonjwa huo wa akili ulisababishwa na matatizo ya kinyumbani. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli. Sivyo? Unaamini sasa? [Dada huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Basi nenda zako ukayakute jinsi unavyoamini. Mungu awe pamoja nawe. Kuwa na imani, na uamini. Itakuwa sawa.

268 Mnaamini kwa moyo wenu wote? Hakika. Yeye anajua yote kuwahusu.

269 U hali gani, bwana? Hatufahamiani, nadhani. [Ndugu huyo anasema, "Naam, bwana."—Mh.] Bwana Yesu anatujua sote wawili. Sisi ni wanaume wawili waliokutana hapa kwa mara ya kwanza maishani. Lakini kuna Mtu fulani hapa. Usininii . . .

270 Kutetemeka, huo ni udhaifu tu, unaona. Nilizungumza kwa saa moja ama zaidi; haikunidhuru. Bali ono moja tu, hilo hulifanya. Unaona? Unaona? Ni wangapi wanajisikia mnaelewa hilo? Danieli aliona ono moja, akasumbuka kichwani mwake siku nyingi. Yesu alihubiri usiku kucha na kila kitu, bali maskini mwanamke mmoja aligusa vazi Lake ndipo Yeye akasema, "Naona ya kwamba nguvu zimenitoka." Hiyo ni kweli? Huo ni uweza. Na kama itafanya hivyo kwa Mwana wa Mungu, ingefanya nini kwangu mimi, mwenye dhambi? Mnaona? Mnaona? Inakufanyia jambo fulani. Kwa kweli, wasikilizaji wote sasa wanaonekana kuingia ukungu. Unaona?

271 Sikujui wewe, bali Mungu anakujua. Lakini kama atanifunulia kilicho moyoni mwako, basi Yeye . . . Yesu aliyatambua mawazo yao yenyewe. Unaona? Yeye anaujua moyo wako. Na kama anaweza kukufunulia shauku zako, ungeamini ungezipokea? [Ndugu huyo anasema, "Amina."—Mh.]

272 Ni wangapi huko nje wangeamini mngezipokea? Hilo linapaswa kulitatua, kama mnaliamini.

273 Kitu fulani mkononi mwako kinaonyesha una shinikizo kuu la damu. Hiyo ni kweli. Lakini lina chanzo, na chanzo hicho ni kumea kwa tezi. Hiyo ni kweli. Unaniamini Mimi kuwa ni nabii Wake, au mtumishi Wake, hasa? [Ndugu huyo anasema, "Naam, bwana. Ninaamini."—Mh.] Unaamini Yeye anakujua? ["Amina."] Unataka uponywe kwa sababu nzuri. Unataka kuwa mmishenari. Kituo chako kitakuwa Marekani ya Kati. Hiyo ni kweli? Bw. Ogum, amini kwa nafsi yako yote, amini kwa moyo wako wote. Nenda ukapokee uponyaji wako. Yesu Kristo atakupa afya.

274 Mnaamini? Ni wangapi wanaamini ya kwamba Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Mnaamini Yeye yupo hapa?

275 Sasa hebu niwape Andiko lingine. Yesu alisema, "Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; yeye asiyeamini atahukumiwa. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Hiyo ni kweli? "Katika Jina Langu watatoa pepo. Watanena kwa lugha mpya. Kama wakishika nyoka au kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Ni wangapi wanajua hilo ni kweli?

276 Maneno Yake ya mwisho yaliyoanguka kutoka midomoni mwake yalikuwa yapi wakati akichukuliwa juu? "Wakiweka

mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Hiyo ni kweli? Mnaliamini hilo? Ni waaminio wangapi walio hapa ndani? Hebu tuone. Sawa.

277 Sasa, kama mkitaka kuona mwujiza wa Mungu, aminini ya kwamba haya ninayowaambia, na mnayoyaona yakidhihirishwa, ni Yesu Kristo. Na kisha muweke mikono yenu mmoja juu ya mwingine. Wekeni tu mikono yenu mmoja juu ya mwingine. Haijalishi kuna tatizo gani, weka tu mikono yako juu ya mtu fulani aliye karibu na wewe.

278 Sasa, mnaona, si mimi tu. Ni ninyi. "Ishara hizi," haikusema, "zitamfuata tu William Branham." Ilisema, "Zitafuatana na *hao* waaminio, kama *wa*kiweka mikono *yao* juu ya wagonjwa."

279 Sasa mmeridhika ya kwamba Yesu yu hai na miongoni mwetu? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mbona, Yeye aliyeifanya ahadi hiyo yupo hapa. Sasa wewe mwombee mtu huyo uliyemwekea mikono yako. Unaona? Wewe waombee. Unaona? Usijiombee mwenyewe. Wewe waombee, kwa sababu wanakuombea. Mnaona? Sasa, mnajua Yeye yupo hapa. Yeye alifanya ahadi. Na kama atasimama hapa mbele ya watu na kulihakikisha na kulithibitisha, ya kwamba ni kweli, basi wewe liamini kwa moyo wako wote.

280 Sasa ninaenda kuwaombea ninyi nyote. Basi wakati mnapoombeana, hebu tuamini kwa mioyo yetu yote sasa.

281 Baba yetu wa Mbinguni, sisi, kwa kweli, mioyo yetu imesisimka. Wewe upo hapa usiku wa leo. Hakuna mahali duni kupita kiasi, hakuna mahali pakubwa kupita kiasi, hakuna mahali mbali sana, ila ambapo Wewe utakuja kwa watoto Wako waaminio. Ee Mungu mkuu wa Mbinguni, Wewe umemtuma Yesu Kristo katika umbo la Roho Mtakatifu, ambaye yupo hapa sasa, na anajitambulisha Mwenyewe yeye yule jana, leo, na hata milele, nao watoto wanaamini hilo. Nimewapa Neno Lako. Wewe umelithibitisha Neno Lako.

282 Sasa kunao wengi wagonjwa hapa. Nao ni—wamesisimkwa. Wana furaha. Wana mikono yao, hawa waaminio, watoto hawa waaminio wameweka mikono yao juu ya ndugu au dada yao mgonjwa. Wanaamini. Wanamwombea ndugu ama dada. Na, Mungu, Wewe ulifanya ahadi. Ni Neno Lako.

283 Sasa, kama mtumishi Wako, nimeifikisha ibada hii mahali hapa kusudi sisi, kama waaminio, tuje tukampe ibilisi changamoto, kwamba yeye ametudanganya kila mahali kufikia kiasi atakachotudanganya. Tunaamini ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na Yeye yu hai na yupo hapa pamoja nasi usiku wa leo. Na sisi tunafuata amri Zake, kwa kuwekeana mikono mmoja juu ya mwingine.

284 Shetani, waachilie. Toka ndani yao, katika Jina la Yesu Kristo. Acha kusanyiko hili la watu liende, kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Waachilie, Shetani. Tunakuapisha, kwa Uwepo wa

Yesu Kristo, Yule aliye hai, Mwana wa Mungu aliyefufuka. Waache waende. Na utoke ndani yao, kwa ajili ya utukufu wa Mungu, katika Jina la Yesu Kristo.

285 Kila mtu aliyepo, ambaye, anajisikia ya kwamba Yesu Kristo ametimiza Neno Lake, kwamba Yeye amekuja miongoni mwetu, kwamba Yeye yupo hapa kwa sababu aliahidi kuwa hapa! Yupo hapa na amejitambulisha Mwenyewe. Ni Bwana Yesu yeye yule aliyetembea Galilaya, nawe unaamini ya kwamba Yeye hutimiza Neno Lake lote. Na kwa sababu mtu fulani, mwaminio, alijitambulisha na wewe, kwa kuweka mikono yake juu yako, kujitambulisha mwenyewe pamoja na Neno la Mungu, kwamba wewe sasa umeponywa. Nawe unachukia Shetani kukushikilia muda mwingi zaidi. Imani yako imeachiliwa, kuamini ya kwamba Mungu yupo hapa kutimiza Neno Lake.

286 Simama kwa miguu yako na ukubali uponyaji wako. Wote wanaoliamini, simameni kwa miguu yenu. Jina la Bwana libarikiwe! Inueni mikono yenu na kumsifu, sasa. Mmeponywa katika Jina la Yesu Kristo.

Vema, Tony, njoo.

63-0604 Yesu Kristo Yeye Yule
Jana, Leo, Na Hata Milele

Ramada Inn

Tucson, Arizona Marekani

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org